Iwe Nuru

# MISINGI YA USHIRIKA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI

UMOJA WA WANAWAKE MAKANISA YA WABATISTI

Wafanya Kazi pamoja na Mungu

Iwe Nuru

# MISINGI YA USHIRIKA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI

Iwe Nuru

# MISINGI YA USHIRIKA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI

Published by
Kenya Baptist Media
P.O. Box 30370
Nairobi, Kenya

© Copyright, 1996
Kenya Baptist Media
P.O. Box 30370
Nairobi, Kenya

All rights reserved

# Yaliyomo


**Somo ........................................ Ukarasa**

**Utangulizi ........................................ 4**

**1. Kwa Nini Tunahitaji Kuokolewa? .......................... 5**

**2. Biblia ni Nini? .......................................... 9**

**3. Maombi ni Nini? ........................................ 13**

**4. Je, Mimi ni Wakili Mwema? ............................ 17**

**5. Kanisa ni Nini? ........................................ 21**

**6. Kwa Nini Tunabatiza na Kula Meza ya Bwana? ............ 25**

**7. Ninaweza Kufanya Kazi Gani Katika Kanisa Langu? ........ 29**

**8. Ni Nani Ataenda na Kuwafanya Wengine Kuwa Wanafunzi?.. 33**

**9. Nitatoa Ushuhuda Wangu Vipi? .......................... 37**

**10. Je! Uko Tayari Kushuhudia? ............................ 41**

**11. Je, UWW/WMU ni Nini? ................................ 45**

**12. Shabaha Zetu ni Zipi? ................................ 49**

**13. Wanawake Wabatisti Wanaungana! ........................ 53**

**Kadi za Kifungu cha Kukumbuka ............ Ukarasa wa Katikati**

**Alama ya Wanawake Wabatisti .............. Ukarasa wa Katikati**

**Mpango wa Mungu wa Wokovu ................ Nyuma ya Kitabu**

# UTANGULIZI

Vitabu vya *Iwe Nuru* vimeandikwa kuwafunza na kuwatia nguvu wanawake katika Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili (UWW au Ushirika). Wanawake wa Kenya na Tanzania hutumia *Iwe Nuru* kama kitabu cha mafundisho katika mikutano yao ya kila juma.

***Misingi ya Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili*** kinachukua nafasi ya kitabu cha ***Mipango ya Ushirika Mpya***. Kitabu hiki kipya kitakuwa mwongozo mzuri wa wanawake katika makanisa mapya na ya zamani. Washiriki wapya wanaweza kujifunza mengi zaidi kuhusu wokovu na uhusiano wao na Mungu. Watajifunza juu ya imani ya Wabatisti na mipango yao. Masomo matatu ya mwisho yanaeleza mipango ya Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili. Wanawake ambao wamekuwa katika Ushirika kwa miaka mingi watapata faida kwa kujifunza kitabu hiki. Watahimizwa kumtumikia Kristo vizuri zaidi. Utumishi huu utatokana na kukumbuka imani yao, kusudi na shabaha ya Ushirika.

Kila somo linaanza na **Maandiko ya Biblia**. Vifungu hivi vitakusaidia kuelewa fundisho la Biblia kuhusu somo hilo. Kila somo lina **Kifungu cha Kukumbuka.** Tunaweka maneno ya Mungu mioyoni mwetu (Kumbukumbu la Torati 6:6-7) kwa kukariri vifungu vya Biblia. Tunaweza kufanya hivyo kwa kusoma Biblia kila siku. Mwisho wa kila somo kuna **Vifungu vya Kusoma Juma Hili.**

Panga mikutano ya Ushirika kulingana na mahitaji ya kikundi chako. Mikutano hii ni nafasi ya kuabudu na kuomba. Ni nafasi ya kujifunza zaidi jinsi ya kumtii na kumtumikia Mungu. Anza kila mkutano kwa maombi na kumaliza kwa maombi. Wanawake wengi hufurahia kuimba kabla ya kuanza somo na kuomba. Wasaidie wanawake kujifunza **Vifungu vya Kukumbuka**. Fanya hivi kwa kuvirudia pamoja wakati wa mkutano.

Usisome tu somo wakati wa mikutano. Waulize wanawake tofauti kueleza kila sehemu ya somo. Waulize wengine wasome vifungu vilivyo katika somo.

Katika kila mkutano toa nafasi ya kutaja mambo ya shukrani au ya kuombea. Toa wakati wa matangazo na sadaka ya Ushirika.

Somo La Kwanza

# *KWA NINI TUNAHITAJI KUOKOLEWA?*

**Maandiko ya Biblia:** Mwanzo 3:1-24; Yohana 11:25-27

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."* Yohana 3:16

**Kiongozi:** Tunapoanza kujifunza na kufanya kazi katika Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili tunahitaji kufikiri juu ya uhusiano wetu na Mungu. Yohana 3:16-17 inasema, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye." Kwa nini Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni? Kwa nini tunahitaji kuokolewa? Hebu tutazame Biblia zetu tupate kuelewa vizuri zaidi.

## Mungu Ndiye Muumba wa Vitu Vyote

(Waulize wanawake wanne wasome vifungu vifuatavyo: Mwanzo 1:1-8, 9-19, 20-25 na 1:26-2:3). Biblia inasema, hapo mwanzo wa wakati, Mungu alikuwako. Mungu akaumba mbingu na nchi na vyote vilivyo hai. Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake, mwanadamu akawa bora kuliko viumbe vyote. Mungu alimpenda mwanadamu na akampa mamlaka juu ya viumbe vingine vyote vilivyo hai. Pia alimpa mwanadamu mamlaka ya kuchagua kati ya mema na mabaya. Mungu pia alimuumba mwanadamu ili awe na ushirika naye.

(Chagua mtu mmoja asome Mwanzo 3:1-6.) Mungu alimpa mume na mke mahali pazuri pa kuishi. Lakini Shetani, adui wa Mungu, akawajaribu wakakosa kumtii na wakamwasi Mungu. Hii ilikuwa dhambi yao ya kwanza na uhusiano wao na Mungu ulivunjika. Mume na mke wa kwanza walilazimika kuacha makao yao. Tangu wakati huo walilazimika kufanya kazi kutimiza mahitaji yao. Walilazimika kuendelea kutoa dhabihu au sadaka ya kuteketezwa ili kupokea msamaha wa dhambi zao. Msamaha ulikuwa njia ya pekee ya kuwaruhusu kuendelea kuwa na ushirika na Mungu.

## Mungu Alimtuma Mwanawe

Miaka mia mingi ilipita na kulikuwa na watu wengi ulimwenguni. Kiasi kikubwa cha watu walikuwa wamemsahau Mungu na walikuwa waovu sana. Watu wachache tu ndio waliompenda Mungu na kumtumikia.

Mwisho, Mungu aliamua kumtuma Mwanawe aishi ulimwenguni na kufa kwa ajili ya dhambi za watu. Katika Mathayo 1:21, malaika wa Bwama anasema, "Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao." Kwa hiyo Yesu, Mwana wa Mungu asiye na dhambi alizaliwa na akaishi ulimwenguni kwa miaka 33 akiwa mwanadamu. Yesu alizungumza na wote waliokuwa tayari kupokea ujumbe wa Baba yake wa mbinguni. Sehemu ndogo ya watu ndiyo iliyomfuata. Mwisho, alisulubiwa na kufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Yesu alipokufa msalabani, aliteseka na kufa kwa ajili ya dhambi za watu wote, pamoja na wewe na mimi. Lakini alishinda kifo na siku ya tatu akafufuka kutoka kaburini. Kwa hakika, alikuwa ndiye Mwokozi na angeishi milele. Baadaye Yesu alirudi mbinguni kuwa na Baba yake. Tangu hapo, mwanadamu akawa hana haja ya kutoa dhabihu au sadaka ya kuchomwa ili apate msamaha wa Mungu. Mungu alikuwa amemaliza kumtoa Yesu kuwa dhabihu ya kulipia dhambi za mwanadamu.

Sasa tuangalie maneno ya Yesu katika Biblia. Katika Yohana 14:6, Yesu akamjibu "Mimi ndimi ___________, na ____________, na __________________; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."

Yesu anazungumza na rafiki aitwaye Martha katika Yohana 11:25-26. (Wasomee washiriki maandiko haya.) Je, Yesu anamuuliza nini Martha katika mwisho wa vifungu hivi?

Sasa tusome Yohana 11:27, tupate jibu la Martha. Je, unaweza kujibu swali la Yesu kama alivyojibu Martha? Je, umemwamini au kumkubali Yesu? Je, unatumaini kuwa utapata uzima wa milele?

## Nifanyeje Nipate Kuokolewa?

Tumejibu swali la kwa nini ni lazima tuokolewe. Sasa tuulize swali hili "Nifanyeje nipate kuokolewa?"

Tukitaka kumwamini Yesu, ni lazima kwanza tukubali kuwa tu wenye dhambi. Warumi 3:23 inasema, "Wote wamefanya dhambi, na

kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Ni lazima tukubali kuwa wenye dhambi wanelekea kifoni. Mungu hataki tutengane naye. Kwa hiyo ametoa zawadi ya uzima wa milele. Warumi 6:23 inasema, "Kwa maana mshara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

Mungu anatupenda na anatupa mpango wa jinsi ya kupokea zawadi ya uzima wa milele. Kuonyesha kuwa mtu amepokea zawadi hii ni lazima amkubali Yesu Kristo. Ebu tusome pamoja Yohana 3:16, *Kifungu cha Kukumbuka* cha juma hili. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

Kuonyesha kuwa mtu amepokea mpango huu wa Mungu ni lazima akiri dhambi zake. Akubali kuwa yeye ni mwenye dhambi, ahuzunikie dhambi zake na amwombe Mungu msamaha. Mtu huyu ni lazima amwombe Mungu atawale maisha yake. Yohana wa Kwanza 1:9 inasema, "Tukiziungama dhambi zetu, basi, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

Baada ya hivyo ni lazima mtu aamini kuwa Mungu ametimiza alivyoahidi. Ni lazima aamini kuwa amesamehewa dhambi zake na kupokea uzima wa milele. Tunaambiwa katika Warumi 10:9-10, "Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."

Ni lazima imani yetu na tumaini letu liwe kwa Yesu. Ni sharti tuamini kuwa yeye ndiye Mwana wa Mungu wa kweli na aliye mkamilifu; bila dhambi. Ni lazima tuamini kuwa ametakasa mioyo yetu kwa kuondoa dhambi na kutupa uzima wa milele. Unaposema "naamini," katika moyo wako Yesu atakuwa nawe milele. Katika Yohana 10:27-28 anasema, "Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu."

## Mkristo Ni Kiumbe Kipya

Ebu tusome 2 Wakorintho 5:17. Kifungu hiki kinasema nini kuhusu mtu aliye ndani ya Kristo au aliyeunganishwa naye? Mara tu

tunapomwamini Yesu awe Mwokozi, tunafanyika watu wapya. Kristo huingia ndani ya mioyo yetu na kuishi ndani yetu. Sasa ni lazima tuwe na ushirika na Mungu kupitia kusa Mwanawe, Yesu. Tunaweza kumuuliza atusaidie kumfuata na kumtumikia kila siku. Si rahisi, lakini tunajua atatusaidia.

Sisi tulio Wakristo, ni lazima tumfuate na kumtii Yesu kila siku. Ni lazima tumfanye Kristo kuwa wa kwanza maishani mwetu, na tusiishi maisha ya kujipendeza wenyewe. Yesu alisema, "Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu" (Yohana 12:26). Tukimfuata Yesu atatuongoza siku zote. Tikisoma na kujifunza Neno la Mungu tutaelewa jinzi ya kumtumikia.

**Kiongozi:** Ni lazima tufanye nini tuweze kuokolewa? Ni lazima tujue kuwa tu wenye dhambi. Mungu hataki dhambi zetu zitutenge naye. Anataka kutusamehe na ametoa zawadi ya uzima wa milele kwa njia ya Yesu. Ni lazima tumwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ili tupokee zawadi hii ya uzima wa milele. Halafu, tumwulize Mungu atusamehe dhambi zetu na kumuuliza Kristo aingie na kukaa mioyoni mwetu. Ni lazima sasa tuamini tumefanyika watoto wa Mungu.

Je, unakumbuka Yesu alivyomwambia Martha katika Yohana 11:25-26? "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufu kabisa hata milele." Halafu akamuuliza Martha, "Je! unayasadiki hayo?"

Je, unaweza kujibu kama alivyojibu Martha? Je, unaweza kusema, "Ndiyo, Bwana! Mimi naamini." Tuinamishe vichwa vyetu na tuombe. (Huu ni wakati maalum wa wanawake wa kikundi chako. Waongoze wasio Wakristo wamwulize Yesu aingie katika mioyo yao awe Mwokozi. Waongoze walio Wakristo wamwulize Mungu awasaidie wamfuate na kumtumikia. Wape wanawake nafasi ya kusema "Ninaamini.")

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** Mwanzo 1; **Siku 2)** Mwanzo 2; **Siku 3)** Mwanzo 3;
**Siku 4)** Mwanzo 4; **Siku 5)** Mathayo 7:7-12;
**Siku 6)** Mathayo 16:24-28; **Siku 7)** Warumi 3:21-26

Somo la Pili

# *BIBLIA NI NINI?*

**Maandiko ya Biblia:** Kumbukumbu la Torati 6:5-9; 2 Timotheo 3:16-17

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu."* Zaburi 119:105

**Kiongozi:** Tulisoma katika somo letu lililopita kuwa tunaweza kujifunza jinsi ya kumtumikia na kuwaeleza wengine ujumbe wake. Tunajifunza jinsi ya kumtumikia kwa kuwaonyesha wengine upendo wake na wokovu kwa kusoma na kujifunza neno lake. Tunayapata wapi maneno haya ya Mungu? Tunayapata katika Biblia. Tutajifunza leo yale Wabatisti wanayoamini kuhusu Biblia. Pia tutajifunza kuielewa Biblia na umuhimu wake kwetu tunapoitumia.

Ebu kwanza, tujibu swali lingine. Ni nani mwandishi wa Biblia? Tusikilize jinzi wawili kati ya waandishi wa Biblia walivyojibu swali hili. Tusome 2 Petro 1:20-21. Petro anasema kuwa Biblia si maneno ya mwanadamu. Anasema kuwa maneno yaliyomo katika Biblia ni maneno ya Mungu ambayo Roho Mtakatifu aliwaongoza watu kuyaandika. Katika 2 Timotheo 3:16 (Kisasa), Paulo aliandika, "Maandiko yote Matakatifu yameandikwa kwa uongozi wa Mungu."

Vitabu 66 vya Biblia viliandikwa nyakati tofauti na watu tofauti. Kati ya walioandika, kulikuwa na wachungaji wa mifugo, wakulima, wafalme, wavuvi na walimu.

Biblia imegawanywa katika sehemu mbili, Agano la Kale na Agano Jipya. Neno hili "Agano" lina maana ya mkataba au makubaliano. Kuna orodha ya vitabu vya Biblia katika mwanzo wa Biblia yako . Tuangalie pamoja katika ukurasa huo unaoitwa **Yaliyomo** katika baadhi ya Biblia.

## Agano la Kale

Agano la Kale ni hadithi ya watu wa Mungu kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Sehemu hii inaeleza juu ya makubaliano au uhusiano kati ya Mungu na Wayahudi kabla ya kuja kwa Kristo.

Vitabu vitano vya kwanza katika Agano la Kale ni *vitabu vya sheria*. Vitabu hivi, Mwanzo hadi Kumbukumbu la Torati, viliandikwa na Musa. Vitabu vifuatavyo kumi na viwili, Yoshua hadi Esta, vinaeleza *historia* ya Waebrania. Vitabu vitano vinavyofuata hivi, Ayubu hadi Wimbo Ulio Bora, ni *mashairi na maandiko ya hekima.* Isaya mpaka Malaki, vitabu vyote pamoja ni kumi na saba, vilivyoandikwa na *manabii* na vinaeleza habari za manabii. Manabii hawa walieleza habari za kuja kwa Mwokozi.

## Agano Jipya

Agano Jipya huanza na kuzaliwa kwa Yesu, na kueleza maisha na mafundisho yake. Agano Jipya hueleza habari za mkataba mpya au makubaliano kati ya mwanadamu na Mungu kupitia kwa Yesu. Pia katika Agano hili kuna matendo na mafundisho ya baadhi ya wafuasi wa Yesu. Taja vitabu vinne vya kwanza katika Agano Jipya. 1)__________________ 2)________________ 3)_____________
4)__________________

Vitabu hivi huitwa *Injili* (Habari Njema). Vinaeleza habari za maisha na mafundisho ya Yesu alipokuwa ulimwenguni.. Kitabu cha *Matendo* hueleza jinsi Roho Mtakatifu alivyowaongoza mitume, na Wakristo wengine, baada ya Yesu kufa na kufufuka.

Paulo ameandika vitabu kumi na vitatu vinavyofuata ambavyo ni Warumi hadi Filemoni. Vitabu hivi ni *barua* alizoandikia makanisa na marafiki. Aliandika kuwasaidia wakue katika maisha yao ya kiroho. Vitabu vinane vinavyofuata, Waebrania mpaka Yuda, ni *barua* zilizoandikwa na watu wengine. Barua hizi ni fupi na zina mafundisho mengi ya maisha ya Kikristo. Kitabu cha mwisho katika Agano Jipya ni Ufunuo wa Yohana. Hiki ni kitabu cha *unabii.* Kinaeleza kuhusu kurudi kwa Yesu ulimwenguni kuwakusanya wafuasi wake.

## Mwongozo wa Mkristo

Sisi Wabatisti, huamini kwamba, ni lazima tujifunze Biblia na kuishi kulingana na mafundisho. Biblia ni sharti iwe mamlaka yetu iliyo kamili na ya mwisho. Biblia ni lazima iwe mahali tunapotafuta majibu ya maswali ili kuamua mambo maishani. Pia inastahili kuwa kiongozi katika mambo yetu yote.

Biblia ni mwongozo wa jinsi ya mtu kuwa Mkristo. Tusome pamoja Waebrania 4:12. Kifungu hiki kinasema, "Neno la Mungu li ___________, tena lina _______________, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili."

Biblia hutuonyesha sababu ya kuitwa wenye dhambi na jinsi tulivyo wenye dhambi. Pia Biblia hutueleza tunachopaswa kufanya ili kutubu na kukubali zawadi ya Mungu ya wokovu. Tuliangalia baadhi ya maandiko haya katika Somo la Kwanza.

Pia Biblia ni mwongozo wetu wa kuishi kama Wakristo. Zaburi 119:9 inasema, "Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako." Tunapata maneno haya ya Mungu katika Biblia.

Paulo naye alieleza jinsi Biblia ilivyo mwongozo wa Wakristo. Tusome 2 Timotheo 3:16. Paulo anasema katika kifungu hiki maandiko yanafaa na ni mazuri kwa mambo gani manne?

1)____________________ 2)____________________

3)____________________ 4)____________________

Katika kifungu kifuatacho, 2 Timotheo 3:17, Paulo anasema kuwa mambo haya yanahitajika "Ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."

Mungu hakutupa tu maneno yake katika Biblia. Alitupa pia misaada ya kutusaidia kuelewa na kutumia neno lake. Wakorintho wa Kwanza 2:12 inasema kuwa kupitia kwa Roho Mtakatifu tunaweza kuelewa yote aliyotupa Mungu. Yesu anasema katika Yohana 14:26 kuwa Roho Mtakatifu atatufundisha mambo yote.

## Kutumia Biblia

Tunatumiaje Biblia kama mwongozo wetu? Watu wengi hufungua Biblia zao Jumapili tu kanisani wanapomsikiliza mchungaji wao. Kama ukila chakula Jumapili asubuhi tu, unafikiri kutatokea nini? Kama vile tunavyohitaji kula chakula kila siku, ndivyo Wakristo wanavyohitaji kusoma Biblia kila siku. Tuipe nafasi ibadilishe maisha yetu.

Mkristo anahitaji kusoma Biblia kila siku. Watu wengi wanapendelea kusoma Biblia wakati mmoja kila siku. Omba kabla ya kuanza kusoma Biblia. Mwulize Mungu akuongoza unaposoma. Mwombe Roho Mtakatifu akusaidie kuelewa unayosoma. Somo Zaburi 25:4-5. Daudi aliombaje?

Weka Biblia yako pamoja na daftari ya kuandikia. Unaposoma andika mambo unayotaka kukumbuka. Pia unaweza kutumia daftari hii siku za Jumapili unapomsikiliza mchungaji. Andika mambo yanayokusaidia kuelewa Biblia vizuri zaidi. Andika mambo yatakayokusaidia kukua katika maisha ya Kikristo. Pia unaweza kuandika maswali unayotaka kumuuliza mchungaji au watu wengine.

Je, unahudhuria masomo ya Biblia katika kanisa lako kila juma? Kila kanisa linastahili kuwa na darasa la masomo ya Biblia kwa kila umri kila juma. Makanisa mengi huwa na masomo haya kabla ya ibada. Mengine pia hutoa nafasi ya masomo ya thiologia (TEE) kwa enezi kwa viongozi. "Thiologia" ni masomo kumhusu Mungu. Kila Mkristo anastahili kujifunza Biblia na kushiriki na wengine kuisoma. Mara nyingi tunaelewa Biblia vizuri zaidi tunaposikiliza wengine wakieleza walivyoelewa maneno ya Mungu.

Njia nyingine ya kusoma Biblia ni kusoma pamoja na jamaa. Soma vifungu vichache vya Biblia ukiwa na wenzako kabla au baada ya kila chakula au mwisho wa siku.

## Neno la Mungu Mioyoni Mwetu

Kila somo katika kitabu hiki linaanza na kifungu cha kukumbuka au kukariri. Kukariri vifungu vya Biblia kunatusaidia kufanya maneno ya Mungu kuwa sehemu ya maisha yetu. Hatuwezi kubeba Biblia siku zote, lakini unaweza kubeba Neno la Mungu moyoni mwako ikiwa umekariri vifungu vya Biblia.

Mungu ametueleza jinzi ya kukumbuka na kutumia maneno yake. Tusome pamoja Kumbukumbu la Torati 6:5-9. Je, unafanya mambo haya? Je, maneno ya Mungu ni mwongozo katika maisha yako? Soma 1 Wathesalonike 2:13. Je, Paulo angalikwambia wewe maneno haya?. Je, Neno la Mungu ndilo "litendalo kazi pia ndani yenu"?

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** 1 Wakorintho 2; **Siku 2)** Waebrania 9:15-20
**Siku 3)** Mathayo 4:1-17; **Siku 4)** Waebrania 5:11-14;
**Siku 5)** Zaburi 119:1-32; **Siku 6** )Zaburi 119:33-56;
**Siku 7)** Zaburi 119:57-80

Somo la Tatu

# *MAOMBI NI NINI?*

**Maandiko ya Biblia:** Mathayo 6:5-15; Yakobo 5:13-18

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani."* Wakolosai 4:2

**Utangulizi wa Kiongozi:** Katika somo letu lililopita, tulijifunza kuwa Biblia ni Neno la Mungu. Mungu anatueleza katika Biblia jinsi ya kuwa Mkristo. Biblia pia ni mwongozo wetu wa kuishi na kukua kama Wakristo. Tunaposoma na kusikiliza maneno ya Biblia tunamsikiliza Mungu mwenyewe. Mungu anazungumza nasi kwa njia nyingine. Njia hii, ni maombi. Maombi pia ni njia tunayotumia kuzungumza na Mungu.

## "Bwana, Tufundishe Sisi Kusali"

Yesu alipoishi ulimwenguni aliitwa mwalimu. Walimu wa siku hizo hawakufundisha katika darasa. Wanafunzi walimfuata mwalimu katika barabara za mji. Walikaa pamoja na mwalimu wao mbali na mji kando ya milima au mito. Walimtazama mwalimu wao, wakamsikiliza na kujifunza kwa kutazama maisha yake. Mara nyingi, mwalimu alifundisha kwa kujibu maswali ya wanafunzi wake.

Tuangalie Luka 11:1-4. Yesu anajibu swali la mmoja wa wafuasi wake. Mathayo pia ameandika mafundisho haya katika kitabu chake. Tusome pia Mathayo 6:9-14.

Yesu anawafundishaje wanafunzi wake kuomba? Yesu alitufundisha tukumbuke kuwa Mungu ni Baba yetu. Anatupenda na anatujali. Tunastahili kujua kuwa ndiye msimamizi wetu na yote tutendayo. Hatumpi amri ya kufuata au kumwambia anachostahili kufanya. Mungu anajua kilicho kizuri maishani mwetu. Kwa hiyo ni lazima tuombe mapenzi ya Mungu yatendeke kwetu.

Tuseme, kwa mfano, uende dukani na kumwambia mwenye duka "Nipe nitakacho." Hivyo si sawa, unamuuliza akupe vitu fulani unavyojua unataka. Pia Yesu alifundisha kuwa tunastahili kuomba vitu tunavyo hitaji au tunavyotaka kwa urahisi na kwa njia iliyo wazi.

Yesu pia alifundisha kuwa katika maombi tunakiri. Alisema tunastahili kuomba msamaha na kuwasamehe wenzetu. Yesu alisema tuombe tulindwe kutoka kwa shetani na nguvu wake.

## "Kufunga Mlango Wako, Usali"

Kumbuka wakati ulipozungumza na rafiki yako unayemwamini kuhusu mambo ya siri ya moyo wako. Je, mlisimama pande mbili tofauti za barabara na kuzungumza kwa kumpazia sauti mwenzio? Je, mlizungumzia mahali ambapo watu wangesikia mazungumzo yenu?

Yesu aliwambia wafuasi wake kuwa hivi ndivyo watu wengi huomba. Tusome Mathayo 6:5-8. Je, Yesu aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini katika Mathayo 6:6. "Bali wewe usalipo, ingia katika ____________ chako cha ndani, na ukiisha ______________ mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini."

Yesu alikuwa akifundisha kuwa kila Mkristo anahitaji wakati maalum wa kuwa pamoja na Mungu. Neno "chumba" linaweza kuwa vyumba tofauti kwa nyakati tofauti. "Chumba" hapa inaweza kuwa chini ya mti au kando ya barabara. Neno "mlango" lamaanisha tunastahili kufunga mlango wa jambo linalotuzuia kuzungumza na Mungu kwa uhuru.

Je, unapozungumza na rafiki yako unayemwamini, unatumia maneno magumu ya kujaribu kumpendeza au la? Soma Mathayo 6:7. Je, tunahitaji maneno magumu na ya kupendeza tunapozungumza na Mungu?

## "Walipo Wawili Watatu Wamekusanyika"

Yesu alifundisha kuwa tunastahili kuomba pamoja. Soma Mathayo 18:19-20. Kifungu cha 20 kinasema, "Kwa kuwa walipo ______________ ________________ wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao." Maneno haya ya Yesu ni ahadi maalum tunayohitaji kukumbuka.

Biblia ina sehemu nyingi ambapo Mungu alipojibu maombi yaliyoombwa na kikundi cha watu. Tusome Matendo 12:5. Tatizo la Petro lilikuwa ni nini? Alipokuwa ____________________. Ni nani aliyekuwa akimwombea? _______________. Sasa soma Matendo 12:11-15. Je, Mungu alijibu ombi lao?

Soma Matendo 4:23-31. Watu waliomba nini katika kifungu cha 29? Waliomba, "Ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote." Je, Mungu alijibu maombi yao?

## "Nawaombea Hao"

Je, unajua kuwa Yesu alikuombea kabla ya kukamatwa na kusulubiwa? Soma Yohana 17:9. Yesu alitufundisha kuwaombea wengine kwa mfano wake. Haya huitwa maombezi au kuombea wengine.

Mara nyingi Paulo aliwaambia marafiki zake kuwa alikuwa anawaombea. Pia aliwauliza wamwombee. Soma vifungu vifuatavyo kutoka katika barua za Paulo. Kila fungu linajibu maswali haya. Je, Paulo aliwaombeaje wengine? Alitaka wenzake wamwombee mambo gani?

1) Warumi 1:8-10 na 15:30-31

2) Waefeso 1:15-20 na 6:19-20

3) 2 Wathesalonike 1:11-12 na 3:2

## "Salini Kila Wakati"

Tunaweza kujifunza zaidi jinsi ya kuomba na mambo ya kuombea katika Biblia. Tusome Yakobo 5:13-18 na tuone mwisho wa barua ya Yakobo. "Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? na ____________. Ana moyo wa kuchangamka? na ____________ ____________. Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? na awaite wazee wa kanisa; nao ________________." Yakobo anasema, "Kuomba kwake mwenye kaki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."

Pia, Paulo alitufundisha jinsi ya kuomba. Alifundisha kuwa tunapoomba hatuko peke yetu. Soma Warumi 8:26-27. Ni nani anayetuombea kwa Mungu? Katika barua nyingine Paulo anasema, "Salini kila wakati kwa nguvu ya Roho. Kesheni bila kuchoka mkisali kwa ajili ya watu wote wa Mungu." (Waefeso 6:18, Kisasa).

Paulo anarudia maneno haya katika barua yake kwa kanisa la Wathesalonike. Soma 1 Wathesalonike 5:16-18. Paulo anasema, "________________ sikuzote; ________________ bila kukoma; ________________ kwa kila jambo."

Paulo anatukumbusha kuwa tunaposali hatupaswi kuomba vitu tu. Soma Wafilipi 4:4-6. Tunapaswa kukumbuka kumsifu na kumshukuru Mungu siku zote. Nyingi ya Zaburi ni maombi ambayo pengine Paulo alikuwa amekariri akiwa mtoto. Soma Zaburi 104:33-34.

## "Bwana Aliufungua Moyo Wake"

Kuna faida nyingi kwa wanawake Wakristo kukutana kila juma. Moja ya faida kubwa kuliko zote ni kwamba wakati huu unaweza kuwa wa kuomba pamoja. Tunaweza kuombea mambo yanayotuhusu sote na kuombeana.

Tumalize somo hili kwa kusoma Matendo 16:13-15. Kikundi hiki cha maombi kilikuwa ndio mwanzo wa moja wapo ya makanisa. Ni akina nani waliokutana katika sehemu hii ya maombi? Watu wengi zaidi watafanyika Wakristo kama Lidia ikiwa wanawake watakutano kuomba.

Kumbuka wakati wote kwamba kuomba pia ni kumruhusu Mungu azungumze nawe. Tenga wakati wa kuwa kimya na kusikiliza wakati wa maombi. Zaburi 46:10 inasema, "Acheni, mjue ya kuwa mimi ni Mungu." Ruhusu wakati wa kimya ili Bwana afungue moyo wako kama alivyofungua wa Lidia.

Pia, kuwa na wakati wa kusoma Biblia, Neno la Mungu. Anaweza na atazungumza nawe ukisoma Biblia. Je, umewahi kusoma kitabu chote cha Zaburi? Ukisoma maombi mengi katika Zaburi yatakusaidia kuelewa jinsi ya kuomba. Pia, uwe msikilizaji unapokuwa na Wakristo wenzako. Mungu anaweza kuzungumza na wewe kupitia kwa mahuburi ya mchungaji wako Jumapili au kupitia kwa rafiki katika Ushirika wako.

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** Zaburi 51; **Siku 2)** Zaburi 57; **Siku 3)** Marko 11:12-25;
**Siku 4)** Luka 18:1-14; **Siku 5)** Yohana 17:1-26;
**Siku 6)** Matendo 2:42-47; **Siku 7)** Matendo 12:1-17

Somo la Nne

# *JE, MIMI NI WAKILI MWEMA?*

**Maandiko ya Biblia:** 2 Wakorintho 8:1-15, 9:6-15

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu."* 1 Wakorintho 4:2

Somo letu la kwanza lilikuwa juu ya zawadi ya Mungu ya uzima wa milele kupitia kwa Yesu Kristo. Halafu tukaangalia zawadi nyingine kutoka kwa Mungu, ambayo ni Biblia. Somo letu la mwisho lilikuwa juu ya maombi na zawadi tuliyo nayo ya kuzungumza na Mungu. Leo tutajibu swali hili, "Je, mimi ni wakili mwema wa vipawa ninavyopewa na Mungu?"

Wakili ni mtu anayetunza mali ya mtu mwingine. Mungu anahitaji tuwe mawakili wazuri wa vitu vyote alivyotupatia. Hii ina maanisha tunastahili kutumia vipawa anavyotupa Mungu, kwa makusudi mema. Ni vipawa ambavyo vinahitaji uwakili mwema?

## Zawadi ya Kwanza ya Mwanadamu Kutoka kwa Mungu

Tunaweza kupata majibu ya swali hili kutoka katika Biblia. Soma Mwanzo 1:26. Ni kitu gani mwanadamu anachopaswa kutunza katika kifungu hiki? (Ngojea majibu kwanza.) Tunatumiaje au tunapata faida gani kutokana na samaki, ndege na wanyama?

Mungu anamshirikisha mwanadamu zaidi katika kuumba katika Mwanzo 2:8-9. Elewa kuwa Mungu hakuumba miti itoe chakula tu. Pia aliumba kila mti "unaotamanika kwa macho". Mungu alitaka tufurahie kutazama na kuutumia ulimwengu alioumba.

Sasa tuangalie Mungu alitarajia nini kutoka kwa mwanadamu. Mwanzo 2:15 inasema Mungu alimtaka mwanadamu afanye nini katika bustani ya Edeni? Mungu alimtaka mwanadamu awe wakili mwema wa zawadi alizokuwa amempa. Mwanadamu alitakiwa kutunza vitu alivyoumba Mungu.

## Zawadi ya Kwanza ya Mwanadamu Kumtolea Mungu

Tunaelezwa katika Mwanzo 4 kuzaliwa kwa wavulana wawili katika jamaa ya Adamu na Hawa. Kaini, mvulana yule mkubwa alikuwa mkulima na Habili akawa mchungaji. Wavulana hawa walipokua kwa umri walimtolea Mungu sadaka. Kaini alileta

matunda kutoka shambani, naye Habili akaleta nyama kutoka kwa wazaliwa wa kwanza wa wanyama wake.

Soma Mwanzo 4:3-8. Tunajifunza mambo mawili katika vifungu hivi. Tunamtolea Mungu shukrani zetu kwa ajili ya zawadi zake kwa kumtoa sadaka. Lakini, zawadi hizi ni lazima zitoke katika moyo unaompenda na kutaka kumheshimu na kumtumikia Mungu. Yohana wa Kwanza 3:12 inasema Kaini aliongozwa na yule mwovu. Matendo yake yalitawaliwa na shetani wala si Mungu.

Biblia inatwambia kuwa watu waliendelea kumtolea Mungu sadaka kama njia ya kumshukuru na kumwabudu. Abramu aliwashinda wale wafalme wanne katika Mwanzo 14. Alimpa kuhani wa Mungu sehemu ya kumi ya mali yake yote. Yakobo mjukuu wa Abram, pia aliahidi kumtolea Mungu sadaka. Alisema, "Na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi." (Mwanzo 28:22)

## Amri za Mungu Zinazohusu Kutoa

Mungu alimchagua Musa awaongoze Wayahudi kutoka Misri kwenda Nchi ya Ahadi. Mungu pia alimchagua Musa awaandikie watu wake amri na sheria. Sheria hizi zilikuwa pamoja na jinsi ya kumwabudu Mungu kwa kumpatia zawadi. Soma Mambo ya Walawi 27:30-33.

Zawadi hizi zilitumiwaje? Kutoka 35:21 tunasoma watu walileta sadaka ili wajenge "hema ya kukutania." Wakati Musa alipoishi, watu waliabudu ndani ya hema. Kifungu hiki kinasema sadaka zao zilitumiwa kununua kila kitu kilicho hitajika kutumiwa katika ibada.

Musa aliandika katika Hesabu 18:21 kuwa Mungu alisema zaka zichukuliwe na Walawi. Walawi ndio waliotunza nyumba ya Mungu na ibada zote. Watu hawa hawangekuwa wakulima au wachungaji. Kazi yao ilikuwa ni kufanya kazi ya Mungu. Zaka ilikuwa ya kutengeneza kazi ya Mungu na wafanyakazi wake. Paulo anarudia mpango huu wa Mungu katika Agano Jipya katika 1 Wakorintho 9:14. Je, tunamlipa mchungaji wetu mshahara wa kutosha? Je, anaweza kutumia muda wake kufanya kazi ya Mungu?

Siku hizi, sadaka zetu bado zinatakikana ili kujenga makanisa yenye nguvu. Labda kwa kununua simiti na mbao za kujenga au

kununua kiwanja. Matoleo yetu pia yanahitaji kununua vitu kama Biblia, vitabu vya masomo, na vitabu vya nyimbo.

Soma Warumi 10:14-15. Sadaka zetu pia zinahitajika kuwatuma wainjilisti sehemu zisizo na makanisa. Tunaweza kuyasaidia makanisa mapya kulipa kodi ya nyumba au mshahara wa mchungaji hadi makanisa hayo yapate nguvu.

## Kutoa kwa Moyo

"Wakaja kila mtu ambaye moyo wake ulimhimiza, na kila mtu ambaye roho yake ilimfanya kuwa apenda, nao wakaleta sadaka za kumpa Bwana." Maneno haya yanatoka kitabu cha Kutoka 35:21. Soma 2 Wakorintho 9:7. Vifungu hivi vinatufundisha kumpa Mungu zaka na sadaka vipi?

Wakati mmoja Yesu aliulizwa ni amri ipi iliyo kubwa kuliko zote. Soma jibu lake katika Mathayo 22:37-39. Wakristo wa mwanzo walielewa maana ya maneno haya. Hawakutoa zaka na sadaka kutii sheria, walitoa kwa ajili ya upendo wao kwa Mungu na jirani zao.

Tunasoma katika Matendo 4:32-37 kuwa hakukuwa na watu wenye mahitaji kati ya waamini. Waamini walishiriki mali yao na wenzao. Waamini matajiri sio tu waliotoa. Soma maneno ya Paulo katika 2 Wakorintho 8:1-5.

## Vipawa Maalum Vitokavyo kwa Mungu

Wakristo wa mwanzo pia walikumbushwa juu ya vipawa vingine ambavyo wangeshiriki na wengine. 1 Petro 4:10 (Kisasa) inasema, "Kila mmoja anapaswa kutumia kipaji alichojaliwa na Mungu kwa faida ya wengine, kama vile wakili mwema wa zawadi mbalimbali za Mungu."

Paulo anaeleza juu ya baadhi ya vipawa hivi katika Warumi 12:6-8. Mungu amekupa kipawa gani unachostahili kutumia "kwa faida ya wengine?" Je, unatumia kipawa hiki?

Paulo aliandika juu ya uwakili mwingine Warumi 12:1-2. Mungu alitupatia miili yetu. Mara nyingi Wakristo wanatumia wakati mwingi wakisaidia wengine na kujisahau. Tunawajibu wa kujitunza mwili na akili.

Pia tuna wajibu wa kukua na kustawi kama Wakristo. Katika Waefeso 4:23-24 (Kisasa) Paulo anasema, "Jirekebisheni upya rohoni na katika fikira zenu. Vaeni hali mpya ya utu ambayo imeumbwa

kwa mfano wa Mungu na ambayo hujionyesha katika maisha ya kweli ya uadilifu na utakatifu."

Tunawezaje kufanya hivi? Tunapaswa kujifunza Biblia na kuomba. Tunapaswa kuwa wafuasi wa Kristo na kufanya aliyotwambia tufanye. Tunaweza kufanya haya ikiwa tutakuwa mawakili wema na watunzaji wema wa wakati. Tusipokuwa mawakili wema hatutapata wakati wa kusoma Biblia, kuomba, na kuhudhuria masomo ya Biblia na ibada. Hatutapata wakati wa kuwatembelea wagonjwa, wenye huzuni na wanaohitaji wokovu.

Pia tunawajibu wa kushirikisha wengine kipawa cha wokovu. Tusome 1 Wakorintho 4:1-2 ambacho kiko pamoja na kifungu chetu cha kukumbuka cha leo.

## Baraka za Kutoa

Tumetoa sababu nyingi za kuwa mawakili wema wa zawadi au vipawa vya Mungu. Ni jinsi tunavyoweza kutoa shukrani zetu kwa Mungu. Ni jinsi tunavyotii amri za Mungu na kuonyesha upendo wetu kwa Mungu. Pia ni sehemu ya ushuhuda wetu kwa wengine kuhusu upendo wa Mungu kwetu.

Kuna sababu nyingine ya kuwa mawakili wema. Soma Malaki 3:10 katika Agano la Kale na 2 Wakorintho 9:6-11 katika Agano Jipya. Mungu anaahidi kufanya nini tukiwa mawakili wema?

Kuna ahadi nyingine katika Yohana 14:21. Yesu alisema, "Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake."

Soma Malaki 3:6-9. Nabii Malaki aliwaambia watu wa wakati wake kuwa walikuwa wanamwibia Mungu. Je, unaweza kusema kuwa wewe ni wakili wa vitu vyote alivyokupa Mungu? Omba sasa na umshukuru Mungu kwa vipawa ambavyo amekupatia. Mwulize akuongonze unapotumia na kutunza vipawa hivi.

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** Mwanzo 28:10-22; **Siku 2)** Malaki 3;
**Siku 3)** Mathayo 6:1-4; **Siku 4)** Mathayo 25:14-30;
**Siku 5)** 2 Wakorintho 8; **Siku 6)** 2 Wakorintho 9;
**Siku 7)** 1 Yohana 3:11-24

Somo la Tano

# *Kanisa Ni Nini?*

**Maandiko ya Biblia:** Mathayo 16:13-18; Waebrania 9

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?"* 1 Wakorintho 3:16

Katika masomo manne yaliyopita tulijifunza kuhusu uhusiano wetu binafsi na Kristo. Tumejifunza juu ya kipawa cha wokovu anachotoa Mungu kwa kumtumia Yesu Kristo. Tumejifunza mambo zaidi kuhusu Biblia, maombi, na jinsi ya kuwa mawakili wema wa vipawa vyote vya Mungu.

Leo tutajifunza jinsi tulivyounganika na watu wengine wamwaminio Yesu Kristo. Soma hili linahusu jinsi Biblia inavyoeleza maana ya kanisa. Katika somo litakalofuata tutaangalia Ubatizo na Meza ya Bwana au Chakula cha Bwana. Hizi ndizo amri mbili ambazo sisi Wabatisti huamini tumeamriwa katika Biblia tuzifuate. Halafu tutatazama wajibu wa kanisa. Pia tutaangalia jinsi Mungu anavyosema kuhusu wajibu wa kila mshiriki kanisani.

## Sehemu za Kuabudia

Katika somo letu lililopita tunasoma katika Agano la Kale kuhusu sadaka ya hema ya kukutania. Mungu alimwambia Musa katika Kutoka 25:8, "Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao." Mungu alimwambia Musa jinsi ya kujenga mahali hapo pa ibada. Pia alimweleza vitu vya kuweka humo ndani. Musa alieleza maelezo haya yote katika Kutoka 25-40.

Mfalme Daudi alifanya mpango wa hekalu kubwa. Lakini mwanawe Sulemani ndiye aliyelijenga. Wafalme wa Kwanza 5-8 na 2 Mambo ya Nyakati 2-7 ni maelezo ya shughuli za kujenga jengo hili la ibada. Mungu alipendezwa na jengo hili. Soma maneno ya Sulemani katika 2 Mambo ya Nyakati 7:1 na 7:11-16.

Agano Jipya linatwambia kuwa Yesu aliingia na kufundisha katika hekalu huko Yerusalemu na katika sinagogi, nyumba za ibada katika miji mingine. Soma Mathayo 9:35. Yesu alihubiria na kufundishia wapi? Soma Mathayo 5:1-2, Marko 2:1-2, Marko 4:1.

Sasa tusome Matendo 16:13. Je, watu hawa walikuwa na ibada na maombi katika jengo zuri lililojengwa kwa ustadi? Walikuwa wakiabudu nje kama makanisa mengi ya Wabatisti wa Afrika ya Mashariki.

Kanisa ni nini? Kwa nini wafuasi wa Yesu waliomba na kuabudu kando ya milima, bahari na ndani ya nyumba za kuishi? Kwa nini Yesu hakuwaambia wakutane katika mahekalu mazuri ya kupendeza kama lile alilojenga Sulemani?

## Mkataba Mpya

Je, unakumbuka maana ya "agano"? Agano ni mkataba au makubaliano. Katika nyakati za Agano la Kale watu walipaswa kumtii Mungu. Walifanya hivyo kwa kufuata maagano kati ya Mungu na Abramu na amri ambazo Mungu alimpa Musa. Amri hizi zilieleza jinsi ya kuabudu na mahali pa kuabudia Mungu.

Agano Jipya linatueleza juu ya mkataba au kukubaliana upya na Mungu. Mkataba huu mpya unafanywa kupitia kwa Yesu. Mmoja wa manabii wa Agano la Kale alitaja agano jipya ambalo Mungu angefanya na watu wake. Soma Yeremia 31:31-34. Yesu ndiye mpatanishi au ndiye anayepanga mkataba huu mypa. Soma Waebrania 9:15.

Katika mkataba wa kale, Mungu aliishi ndani ya mahekalu yaliyojengwa na watu kuwa mahali pa ibada. Katika mkataba mpya, Mungu anaishi ndani ya mioyo ya wote waliokubali kipawa cha wokovu kupitia kwa Yesu Kristo. Soma 1 Wakorintho 3:16 na 6:19-20.

## Walioamini Waliungana

Kwa hiyo *kanisa* ni nini na ni nani? Mara chache katika Biblia *kanisa* linatajwa kuwa wale wote waliomwamini Yesu Kristo. Mara tisini na tatu katika Biblia *kanisa* linatajwa kuwa kundi dogo la watu waliokutana kuabudu na kuhudumu katika jina la Yesu Kristo. Vikundi hivi vya walioamini havikuhitaji mahali maalum pa kukutania. Pia havikuhitaji kuabudu kwa njia fulani ili kumpendeza Mungu. Hawa walioamini walikuwa kanisa kwa sababu ya uhusiano wao na Mungu. Uhusiano ulitokana na kumkubali Yesu Kristo, Mwanawe.

*Sisi Wabatisti huamini kuwa kanisa ni kundi la walioamini na kubatizwa. Walioungana kwa kusudi na hamu ya kutii amri za Yesu.* Waamani hawa walishiriki na kuabudu pamoja. Wanafanya kazi pamoja ili kufanya kazi ambayo Yesu aliwaambia wafuasi wake katika Mathayo 28:19-20. Wao ni wanafunzi wa Yesu wanaowafanya wengine wanafunzi!

Kanisa hili mara nyingi hukutana katika jengo lakini kanisa si jengo. Kanisa ni Wakristo wanaokutana pamoja ili kuabudu, kuwa na ushirika, kutoa ushuhuda na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

Sisi Wakristo si lazima kuwa katika jengo maalum na kufuata sheria fulani ili kuleta haja zetu kwa Mungu. Hatuna haja kumuuliza kuhani au mtu mwingine yeyote kutuombea kwa Mungu. Katika mkataba mpya tunaweza kuomba na kuzungumza na Mungu mahali popote na wakati wowote. Tunaweza kufanya hivi kwa sababu tumepokea kipawa cha wokovu. Tumechagua kuwa wafuasi wa Kristo na kumuuliza Roho wa Mungu kuishi ndani yetu.

## Kanisa Ni "Mwili wa Kristo"

Waandishi wa Agano Jipya walitusaidia kuelewa maana ya kanisa na kwa nini Yesu ni sehemu ya Kanisa. Katika Waefeso 1:22-23 inasema, Mungu "akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake." Paulo anazungumza na kila mmoja wetu alipoandika 1 Wakorintho 12:27, "Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake."

Paulo alisema katika 1 Wakorintho 12 kuwa mwili una sehemu nyingi ambazo zinapaswa kufanya kazi pamoja. Anaeleza kuwa kila mmoja wetu ana vipawa na uwezo fulani. Tunapaswa kuvitumia kufanya kazi aliyotupatia Yesu. Vipawa vyetu na uwezo pekee hautoshi. Tunapaswa kuungana na Wakristo wengine walio na vipawa na uwezo ili kukamilisha kazi aliyotuachia Yesu. Ili kanisa liweze kufanya kazi yake, washiriki wanapaswa kufanya kazi pamoja na washiriki wenzao kwa kutumia vipawa vyao maalum.

## "Nitajenga Kanisa Langu"

Katika Waefeso 2:19-20 Paulo anasema, "Ninyi ni . . . watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni iiwe kuu la pembeni."

Pia Yesu alisema jinsi kanisa lingejengwa. Soma maneno yake katika Mathayo 16:13-18. Petro alijua kuwa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Kanisa lingekuwa wale walioamini kuwa Yesu ni Mwokozi kama Petro alivyofanya. Kanisa lingejengwa juu ya imani yao katika Yesu Kristo. Petro alikuwa bado hajaelewa kabisa yale ambayo yangefanyika baadaye, kwa sababu Yesu alikuwa bado hajakufa msalabani kwa ajili ya dhambi zake. Lakini tayari Mungu alikuwa amegusa moyo wa Petro na kumpa ufahamu maalum kumhusu Yesu.

Mwandishi wa ***"The Doctrines Baptists Believe"*** anasema tunapaswa kukumbuka maneno ya Yesu siku zote katika Mathayo 16:18, "Nitalijenga kanisa langu." Yesu hasemi kanisa lako au kanisa letu. Anasema, "kanisa langu." Wakati mwingine tunasahau kuwa kanisa ni la Yesu na si mali yetu.

## Kanisa Lenye Moyo wa Furaha na Ukarimu

Tunasoma katika Matendo 2 juu ya wakati maalum katika moja ya makanisa ya mwanzo. Matendo 2:42 inasema, "Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali." Biblia inatwambia waliabudu pamoja kila siku. Soma sentensi ya mwisho katika mlango huu Matendo 2:47.

Fikiri juu ya kanisa lako. Kwa nini mnakutana pamoja kila Jumapili asubuhi na nyakati nyingine tofauti? Je, mnakutana kuabudu, kushirikiana, kushuhudia na kuwafanya watu kuwa wanafunzi?

Kanisa katika Matendo 2 walifurahia kuwa pamoja. Watu katika kanisa hili walikuwa na moyo wa furaha na ukarimu. Je, maneno haya yanaeleza tabia ya baadhi ya watu katika kanisa lako? Je, watu wanaweza kusema kuwa kanisa lako ni mali ya Yesu? Tulia sasa na omba uongozi wa Mungu uwe katika kanisa lako.

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** Kutoka 25; **Siku 2)** 2 Mambo ya Nyakati 7;
**Siku 3)** Waebrania 9; **Siku 4)** 1 Wakorintho 12;
**Siku 5)** 2 Wakorintho 3; **Siku 6)** Waefeso 4;
**Siku 7)** Wakolosai 1:1-23

Somo la Sita

# *KWA NINI TUNABATIZA NA KULA MEZA YA BWANA?*

**Maandiko ya Biblia:** Mathayo 3:11-17; 26:17-30

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Na huu ndio upendo: tuenende kwa kuzifuata amri zake."* 2 Yohana 6

Katika somo lililopita tulijifunza kuwa, *"kanisa ni kundi la walioamini na kubatizwa. Walioungana kwa kusudi na hamu ya kutii amri za Yesu."* Leo tutaangalia amri au maagizo (ordinances) mawili ya Yesu ambayo Wabatisti hufuata. Hizi ni amri za Ubatizo na Meza ya Bwana au Chakula cha Bwana.

Ni nini maana ya amri (ordinance) hii? Roy Edgemon anasema katika kitabu chake ***The Doctrines Baptists Believe,*** kuwa ni matakwa au mambo yanayotakikana, mpango au amri iliyo na kusudi na maana.

Amri hii ya Ubatizo na Meza ya Bwana haifanywi ili kumuongezea mtu neema au baraka ya aina fulani. Amri hizi zinafuatwa kwa kuwa Mungu ametuambia tufanye hivyo. Tunafanya mambo haya kumwabudu Mungu. Tunafanya haya ili kukumbuka yaliyopita na kutukumbusha tumaini tuliyonalo ndani ya Kristo. Amri hizi ni wakati wa ushirika pamoja na Wakristo wenzetu. Ni sehemu moja ya ushuhuda wetu kwa walimwengu ambao hawajaokoka. Ni ishara ya thibitisho la upendo wetu na kumtii Mungu.

## Yohana Anambatiza Yesu

Je, unakumbuka wakati malaika Gabrieli alipozungumza na bikira Mariamu? Soma Luka 1:35-42. Mungu alikuwa na mpango maalum kwa mwana wa Elizabeth. Soma maneno ya mumewe katika Luka 1:76-79. Tunamjua mtoto wao kama Yohana Mbatizaji.

Yohana alikuwa "anahubiri kwamba ni lazima watu watubu na kubatizwa ili Mungu awaondolee dhambi" (Luka 3:3, Kisasa). Alimtayarishia Yesu njia, kama nabii Isaya alivyotangulia kusema Yohana angefanya. Unaweza kusoma maneno ya nabii katika Isaya 40:3-5 au Luka 3:4-6.

Ubatizo wa Yesu unatajwa katika Injili zote nne. Ebu tusome Mathayo 3:13-17, Marko 1:9-11, Luka 3:21-22, na Yohana 1:19-34.

Ebu fikiri kuhusu yale Yohana aliyoona na kusikia Yesu alipotoka katika maji. Aliona mbingu zikifunguka. Roho wa Mungu alishuka kama njiwa na akakaa juu ya Yesu. Aliyasikia maneno haya, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye" (Mathayo 3:17). Je, ungelisikiaje kama ungesikia na kuona mambo haya?

## Kwa Nini Yesu Alibatizwa?

Kwa nini Yesu alihitaji kubatizwa? Mr. Edgemon anasema kuwa Yesu alituonyesha mambo kadhaa katika ubatizo wake. Kwanza, Mungu alikuwa anajihusisha na mwanadamu na dhambi zake. Yesu alijua kuwa alikuwa amekuja ulimwenguni ili tusamehewe dhambi zetu na kupata uzima wa milele.

Ubatizo ulikuwa njia ya kuonyesha kuwa alikuwa anaanza huduma yake. Yohana alikuwa amemaliza kutayarisha njia na sasa ulikuwa umebaki wakati wa Yesu kuanza kazi yake ulimwenguni. Yesu pia alionyesha kwamba uhusiano mpya na Mungu ambao Yohana alikuwa akifundisha ulikuwa wa kweli.

Ubatizo wa Yesu pia ulikuwa ni ishara au picha au mambo ambayo yangetokea baadaye. Yesu alipobatizwa alizamishwa kabisa ndani ya maji na akatoka ndani ya maji. Huu ni mfano wa yale yaliyokuwa yakitendeka katika maisha ya Yesu. Angekufa, azikwe na afufuke.

Hii ndiyo picha tunayoonyesha ulimwengu tunapofuata mfano wake wa ubatizo. Soma Warumi 6:3-4. Tunapobatizwa utu wetu wa dhambi unakufa na kuoshwa. Halafu tunafufuliwa au tunaanza kuishi maisha mapya tukiwa wafuasi wa Kristo anayetuongoza.

## Ni Nani Anayebatizwa?

Wabatisti huamini kuwa ni wale tu waliomwamini Yesu wanaostahili kubatizwa. Ubatizo ni njia ya kuuabia ulimwengu, "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu" (Wagalatia 2:20).

Hatuokolewi kwa kubatizwa. Tunaokolewa kwa kukubali mpango wa Mungu wa wokovu ulio katika Yesu. Kwa hiyo, sisi Wabatisti hatubatizi watoto wachanga. Mtoto anapoelewa mafundisho ya Biblia kuhusu wokovu, anapaswa kumkubali Kristo awe Mwokozi wake. Baada ya kufanya hivyo anaweza kubatizwa.

Pia Wabatisti wanaamini kuwa tunapaswa kutumbukizwa au kuwa ndani ya maji tunapobatizwa. Agano Jipya, kwa mara ya kwanza,

iliandikwa kwa Kiyunani au Kigiriki. Neno hili *baptizo* linamaanisha kutumbukizwa, au kuzamisha ndani ya maji. Mathayo 3:16 inasema kuwa baada ya Yesu kubatizwa "akapanda kutoka majini."

## Chakula cha Pasaka

Yesu alibatizwa wakati wa kuanza huduma yake hapa ulimwenguni. Meza ya Bwana ya kwanza ilikuwa wakati wa chakula maalum cha Pasaka masaa machache kabla ya Yesu kukamatwa. Wanafunzi hawakuelewa kile ambacho kingetendeka, lakini Yesu alijua kuwa huduma yake ulimwenguni ilielekea kumalizika. Soma Luka 18:31-34.

Tusome Kutoka 12:1-14. Hadithi hii husimuliwa na Wayahudi wakati wa chakula maalum kukumbuka Pasaka. Maombi na nyimbo ni sehemu moja ya sherehe hizi. Yesu na wanafunzi wake labda waliimba Zaburi 113-118 kama wanavyofanya Wayahudi wakati wa sherehe za Pasaka.

Chakula kilichoandaliwa (kilichotayarishwa) kilikuwa na maana maalum kwa Wayahudi. Mkate usio na chachu uliwakumbusha kuwa waliondoka Misri kwa haraka hata hawakuwa na wakati wa mkate wao kufura. Mimea michungu waliyokula iliwakumbusha mateso makali ya utumwa. Sehemu nyingine ya chakula hiki ilikuwa ni mwanakondoo wa kuchomwa. Jambo hili liliwakumbusha wanakondoo waliotumika kuwaokoa Wayahudi wasife.

## Meza ya Bwana ya Kwanza

Mungu aliwaeleza Wayahudi jinsi ya kusherehekea Pasaka kila mwaka. Alitaka wakumbuke jinsi alivyowaokoa kutoka katika utumwa huko Misri kwa dhabihu ya mwanakondoo. Yesu aliwaonyesha wanafunzi wake jinsi ya kusherehekea Meza ya Bwana. Hii ilikuwa ni njia ya kukumbuka jinsi Mungu alivyookoa watu wake kwa njia mpya. Alikuwa akiwaokoa kutoka katika utumwa wa dhambi. Wakati huu dhabihu ni Mwanawe, Yesu. Tusome kuhusu Meza ya Bwana ya kwanza katika Mathayo 26:20-30.

Je, unaweza kubahatisha walivyojisikia wanafunzi Yesu aliposema, "Yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye atakayenisaliti"? Mwalimu wao alikuwa anaenda kusalitiwa. Wengi wao walikuwa wamechovya mkate pamoja naye. Mmoja wao ndiye angemsaliti!

Kicheko na furaha mezani zilikoma. Chakula ambacho Yesu aliwaandalia wanafunzi wake kikawa cha huzuni sana. Yesu alimega mkate akawapa wanafunzi. Alisema kuwa mwili wake ungevunjwa kama huo mkate. Aliwapa wanafunzi wake divai. Alisema kuwa hii ni damu yake na akataja agano jipya. Wanafunzi hawakuelewa aliyokuwa akisema Yesu.

Wanafunzi walielewa maneno ya Yesu, baada ya Yesu kufa, kuzikwa na kufufuka na kwenda kwa babaye. Hili lilikuwa ni agano au mkataba mapya kati ya Mungu na mwanadamu kupitia kwa Yesu Kristo. Mungu alikuwa na njia nyingine ya mwanadamu kusamehewa dhambi zake na kupata uzima wa milele. Yesu alikuwa ndiye dhabihu. Mwili wake ulivunjwa na damu "imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi."

## Ni Nani Anayestahili Kushiriki Meza ya Bwana?

Mungu alimwambia Musa katika Kutoka 12 kuwa mtu mgeni au anayeishi hapo kwa muda mfupi hastahili kula chakula cha Pasaka. Yesu alipokuwa akila Meza ya Bwana na wanafunzi alisema, "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" (Luka 22:19). Sisi Wabatisti tunaamini kuwa wale tu walioamini ndio wanaostahili kula chakula cha Bwana. Ni wale tu waliookolewa kutoka dhambini ndio wanaoweza kula kwa kumkumbuka Yesu na yale aliyowatendea.

Meza ya Bwana ina maana tu kwa wale walioweka imani yao katika Yesu Kristo. Hawa ndio wanaotaka kufuata mafundisho yake na kufanya yale ambayo Yesu aliwaambia wafanye.

Ubatizo ni njia moja ya kuonyesha ulimwengu kuwa sisi tu wafuasi wa Kristo. Kushiriki katika chakula cha Bwana ni njia nyingine ya kuwaambia wenzetu habari za Mwokozi wetu. Tumalize sehemu hii kwa kusoma 1 Wakorintho 11:26. Ubatizo na Meza ya Bwana ni njia za kukumbuka yale ambayo Yesu alitutendea wakati uliopita. Hizi pia ni njia za kukumbuka siku zijazo. Yesu atarudi na wale wanaomwamini watapata uzima wa milele!

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** Luka 1:5-38; **Siku 2)** Luka 1:39-80; **Siku 3)** Warumi 6:1-14; **Siku 4)** Wagalatia 3:21- 4:7; **Siku 5)** Marko 11:1-19;
**Siku 6)** Marko 14:1-11; **Siku 7)** Zaburi 136

Somo la Saba

# *NINAWEZA KUFANYA KAZI GANI KATIKA KANISA LANGU?*

**Maandiko ya Biblia:** Warumi 12:1-8

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake."* 1 Wakorintho 12:27

Kanisa moja lilikutana kuabudu kwa mara ya kwanza. Karibu na hapa kulikuwa na kiongozi wa kanisa lingine. Mwanamume na mwanamke wa kwanza kufika alimpa kitabu cha masomo ya Biblia. Alimwambia mwanamume afundishe darasa la watu wazima. Naye mama angefundisha watoto. Mwanamke aliyefuata hawa wawili aliambiwa aongoze nyimbo. Aliyefuata huyu mwanamke aliambiwa akusanye sadaka wakati wa ibada katika kanisa hili jipya.

Hali ya ibada haikuwa nzuri Jumapili hiyo! Wale *walimu* hawakuweza kusoma. Mkusanyaji sadaka alikuwa na mkono uliokuwa mdhaifu na kila mara aliangusha chombo cha sadaka. Naye kiongozi wa nyimbo alikuwa akianza nyimbo kwa sauti ya juu sana.

Baadaye watu walizungumza na yule kiongozi mwenye huzuni. Ilidhihirika kwamba mwanamume aliyepewa darasa la watu wazima alikuwa mwimbaji stadi na alijua maneno ya nyimbo zote. Yeye angeweza kuongoza uimbaji. Mkewe aliomba apewe ufunguo wa mahali pa kukutania ili afagie na kuosha. Yule kiongozi aliyeanza nyimbo kwa sauti ya juu na yule aliyekuwa na mkono dhaifu walisema, "Sisi ni walimu na tunaweza kufundisha masomo ya Biblia kila Jumapili."

Soma maneno Paulo aliyowaambia kanisa la Rumi katika Warumi 12:4-8. Anasema kuwa Mungu aliumba kanisa liwe kama miili yetu. Viungo tofauti vinahitaji kufanya kazi tofauti. Mungu amempa kila mmoja wetu uwezo wa aina fulani. Tunapaswa kutumia uwezo huu kusaidia kanisa litende kazi yake.

## Kanisa Nyakati za Yesu

Yesu alianza kanisa kama sehemu moja ya agano au mkatabu kati ya Mungu na mwanadamu. Hakuwapa wafuasi wake taratibu za kupanga vikundi vya kanisa. Alifundisha jinsi ya kumtii na kumtumikia Mungu. Aliwaambia wanafunzi mambo ambayo Mungu alitarajia wafanye. Soma maneno yake katika Mathayo 28:19-20.

Baada ya Yesu kuondoka ulimwenguni, makanisa machanga yalitaka kufanya yale yote alifundisha. Waligundua kwamba ni lazima wafanye mpango wa kushirikiana. Walichagua viongozi wa kazi mbalimbali. Walipanga mipango ambayo ingewasaidia kufanya yote ambayo Yesu alitarajia wafanya.

Mashemasi wa kwanza walichaguliwa kusaidia kanisa lifuate amri za Yesu. Tunaweza kusoma hayo katika Matendo 6:1-7. Kifungu cha 7 kinaeleza kuwa "hesabu ya wanafunzi ikazidi sana." Makanisa yalifanya mipango mizuri ili kufuata mafundisho ya Yesu.

Washiriki wa makanisa ya mwanzo walitaka kujua mambo mengi sana kuhusu kuwa wafuasi wa Yesu. Idadi kubwa ya vitabu vya Agano Jipya ni barua zilizoandikwa kufundisha na kuongoza makanisa haya. Biblia yetu ina barua mbili ambazo Paulo alimwandikia Timotheo. Paulo anamwambia Timotheo afanye nini katika 2 Timotheo 2:2?

## Kanisa Linaongozwa

Je, makanisa yanajuaje jinsi ya kuamua mambo? Tuangalie jinsi makanisa katika Agano Jipya walivyochagua viongozi maalum.

Je, unakumbuka kazi ya Yuda kabla ya kumsaliti Yesu? Tunaambia katika Yohana 12:4-6 na 13:29 alikuwa mtunza pesa za wanafunzi wa Yesu. Baada ya Yesu kwenda mbinguni waumini walichagua mtu mwingine kuchukua kazi ya Yuda. Soma uone jinsi walivyomchagua kiongozi wao mpya katika Matendo 1:23-26. Je, tunaweza kuufuata mfano wao wa kuomba uongozi wa Mungu katika kuchagua viongozi wetu?

Pia, makanisa yalituma waenezaji Habari Njema za wokovu. Katika Matendo 13:1-3, Roho Mtakatifu aliongoza kanisa la Antiokia kusikia maneno haya "Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia."

Makanisa ya Agano Jipya yalifanya uamuzi pamoja. Tunaambiwa katika Matendo 1:15 kuwa ni kile kikundi cha waumini mia moja na ishirini kilicho mteua Mathia kuchukua nafasi ya Yuda. Katika Matendo 6 tunasoma kuwa kikundi cha wanafunzi ndicho kilichochagua mashemasi au wazee. Barnaba na Saulo walichaguliwa na kanisa la Antiokia kuwa waenezaji Habari Njema.

## Shughuli na Mipango ya Kanisa

Waumini waliambiwa katika Waebrania 10:24-25 wasaidiane wapendane na watende matendo mema. Waliambiwa wakutane na kutiana moyo wao kwa wao. Kwa shughuli zilizo na mpango, kanisa letu linaweza kufanya hivi.

Kila kanisa linastahili kutoa nafasi ya madarasa ya masomo ya Biblia kwa umri wote. Biblia ni Neno la Mungu. Ni kitabu cha majibu na mwongozo wa waumini. Makanisa ya Kibatisti yanaweza kutoa nafasi ya masomo ya Biblia kwa kuwa na mpango wa Shule ya Jumapili. Kila umri wa watu unastahili kuwa na madarasa yao, kuanzia yule mdogo kabisa hadi yule mzee sana. Vitabu vya masomo vinaweza kununuliwa kutoka Kenya Baptist Media, S.L.P 30370, Nairobi, Kenya au Baptist Literature Centre S.L.P 1240, Moshi, Tanzania. Jumuiya yako inaweza kukusaidia kupata vitabu hivi.

Washiriki wa kanisa pia wanaweza kufundishwa au kutiwa moyo kupitia katika vikundi hivi vidogo. Wanawake wa kanisa wanastahili kukutana kila juma ili kujifunza, kuomba na kuwa na ushirika. Kanisa linastahili kuwa na vikundi vya wanaume, watoto, na vijana. Masomo zaidi yanastahili kupangwa kwa mfano ETE (Elimu ya Theologia kwa Enezi) na TEE (Theological Education by Extension). Katika vikundi hivi washiriki wanaweza kujifunza zaidi juu ya uanafunzi na jinsi ya kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Washiriki wa vikundi hivi watajua mahitaji ya wengine wanapoelezana mahitaji yao na ya wenzao. Pia wataweza kumtumikia Kristo kwa kuwatembelea wengine wakiwa katika kikundi.

Kikundi cha akina mama katika makanisa ya Kibatisti huitwa *Ushirika Wa Wanawake Waenezao Injili* au *Woman's Missionary Union*. Pia kuna mpango wa watoto uitwao *Wajumbe Wa Yesu.*

Ibada ya Jumapili si chama, lakini ni sehemu muhimu ya kanisa. Ni wakati wa kusikiliza Neno la Mungu na kufikiria maana yake katika maisha yetu. Ni wakati wa kuabudu na kumshukuru Mungu tukiwa na Wakristo wenzetu. Mahudhurio yetu katika ibada hizi ni ushuhuda kwa wengine kuhusu imani yetu kwa Mungu. Makanisa mengi pia hukutana kwa maombi katikati ya juma.

## Jumuiya Ndogo na Kubwa

Makanisa yamegundua kwamba kuwa na ushirika na makanisa mengine kunaweza kuwasaidia kuwa na nguvu. Makanisa ambayo yameungana yanaweza kusaidiana kutii amri za Yesu.

Makanisa ya Kibatisti ni sehemu moja ya **jumuiya ndogo** na **jumuiya kuu**. Jumuiya ndogo ni kikundi cha makanisa ya Wabatisti katika taifa yanayokubaliana na imani yetu. Jumuiya kuu ni makanisa ya Kibatisti katika nchi yetu ambayo yanokubaliana na imani yetu.

Jumuiya kuu au ndogo haina mamlaka juu ya kanisa. Makanisa katika jumuiya ndogo na kubwa yanaungana kusaidiana na kutiana moyo. Wanasaidiana kwa kuwajulisha wengine yale wanayojua ya kumtumikia Mungu. Kwa kufanya kazi pamoja katika kikundi kikubwa kanisa laweza kupata njia mpya na nzuri kufuata amri za Yesu katika Mathayo 28:19-20.

## Kutayarisha Watu wa Mungu Kutumika

Katika barua yake kwa waamini wa Rumi, Paulo alisema waumini wana vipawa maalum. Anaeleza sababu ya Mungu kuwapa waumini vipawa maalum katika barua yake kwa kanisa la Efeso.

- "Kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo" (Waefeso 4:12, Kisasa).
- "Tuwe watu waliokomaa na kuufikia utimilifu wake Kristo mwenyewe" (Waefeso 4:13, Kisasa).
- "Kila kiungo kikitekeleza kazi yake ipasavyo, mwili wote hukua na kujijenga katika upendo" (Waefeso 4:16, Kisasa).

Angalia Warumi 12:6-8 tena. Je, unatumia vipawa vyako kutoka kwa Mungu? Je, unaeleza wengine ujumbe wa Mungu. Je, una kipawa cha utumishi, kufundisha na kuhimiza? Je, unatumia kipawa hiki katika kanisa lako? Je, unatimiza mahitaji ya wengine? Je, una kipawa cha uongozi? Je, wewe ni kiongozi katika kanisa lako? Je, una kipawa cha kuhurumia wengine? Je, unatumia kipawa hiki kwa furaha?

Paulo aliandika katika Warumi 12:10-12 (Kisasa), "Pendaneni kidugu; kila mmoja amfikirie kwanza mwenzake kwa heshima. Msilegee katika bidii, muwe wachangamfu rohoni katika kumtumikia Bwana. Tumaini lenu liwaweke daima wenye furaha; muwe na saburi katika shida, na kusali daima." Je, vifungu hivi vinaeleza tabia ya kanisa lako? Je, wanaweza kueleza kuwa umeamini na u mshiriki wa kanisa? Fanya yale asemayo Paulo na uombe. Omba sasa na mwulize Mungu akusaidie kufanya wajibu ukiwa mtumishi.

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili: Siku 1)** Mathayo 25:31-46; **Siku 2)** Matendo 2:42-47; **Siku 3)** Matendo 11:19-30; **Siku 4)** Matendo 14:21-28; **Siku 5)** 1 Wakorintho 12:1-11; **Siku 6)** 1 Wakorintho 12:12-31; **Siku 7)** Waefeso 4:1-16

Somo la Nane

# *NI NANI ATAENDA NA KUWAFANYA WENGINE KUWA WANAFUNZI?*

**Maandiko ya Biblia:** 2 Wafalme 5:18; Matendo 26:19-32

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari."* *Mathayo 28:19-20*

Katika somo hili tutajifunza juu ya umisheni au kazi ya kueneza Injili katika Biblia. Je, umisheni au kazi maalum ya Wakristo ni nini? Katika Mathayo 28:19-20, Yesu alisema tuwafanye watu wote kuwa wanafunzi katika kila sehemu.

Umisheni wetu au kazi yetu ni kuwaambia wengine yale aliyotutendea Mungu. Tuwaonyeshe wengine upendo wa Mungu na kuwasaidia waukubali wokovu anaotoa Mungu. Katika sehemu nyingi za Biblia tunapata ujumbe huu. Mungu anapenda watu wote. Anawataka watu wote kila mahali waokolewe. Anawauliza wafuasi wake wawe wajumbe wake ili wamshuhudie yeye.

## Ujumbe wa Uenezaji Injili Katika Agano la Kale

Kitabu cha Zaburi ni kitabu cha nyimbo katika Agano la Kale. Vifungu vingi katika Zaburi au nyimbo vinatueleza juu ya wokovu wa Mungu kwa watu wote. Pia nyimbo hizi ziliwakumbusha watu wa Mungu kuwa walikuwa na wajibu wa kueleza watu juu ya neema ya Mungu iokoayo. Nyingi ya Zaburi hizi ziliandikwa na mfalme Daudi. Daudi anaitwa shujaa wa vita, lakini aliulizwa kumtumikia mfalme Sauli kwa sababu ya kipawa chake cha uimbaji (1 Samueli 16:17-18).

Mojawapo ya mambo Daudi alifanya akiwa mfalme ilikuwa ni kutayarisha mahali pa ibada Yerusalemu. Aliandika wimbo au Zaburi ya shukrani itumike katika ibada ya kwanza katika sehemu hii. Tusome sehemu moja ya wimbo huu unaopatikana katika 1 Mambo ya Nyakati 16:23-33. Zaburi hii imeandikwa tena katika Zaburi ya 96.

Je, unasikia ujumbe wa umisheni katika wimbo huu? Zaburi 96:2-3 katika Biblia takatifu inasema, "Tangazeni wokovu wake siku

kwa siku. Wahubirini mataifa habari za utukufu wake, na watu wote habari za maajabu yake."

Soma Zaburi 67. Daudi anauliza watu wa Mungu wabarikiwe ili wawe mashahidi kwa wengine juu ya wokovu wa Mungu. Zaburi hii inatukumbusha sote tunaoimba na kusoma kuwa watu wengine wanaangalia waone Mungu anavyowabariki watu wake. Wanaangalia tunapomsifu na kumwabudu. Wanaweza kujifunza na kukubali wokovu wake kutokana na ushuhuda wetu.

## Mmisheni Katika Agano la Kale

Tunasoma katika 2 Wafalme 5 hadithi ya msichana mdogo mtenda kazi kutoka Israeli ambaye alieleza imani yake kwa afisa wa kijeshi aliyekuwa mgonjwa. Naamani aliongoza jeshi lipigane na Waisraeli, wateule wa Mungu. Msichana huyu mdogo alichukuliwa kama mtumwa na jeshi la afisa huyu na akawa mfanyi kazi wa nyumbani. Alimtumikia mkewe Naamani. Naamani alikuwa kiongozi mashuhuri lakini alikuwa na ukoma.

Huyu msichana alimwambia mkewe Naaman juu ya mtu wa Mungu katika nchi yake. Alisema kuwa Naaman angeweza kuponywa ukoma wake. Mambo mawili yalitokea kwa ajili ya ushuhuda wa huyu msichana mdogo. Mungu alimtumia nabii, Elisha, kumponya Naamani. Bwana wake alijifunza pia kuhusu Mungu wa kweli. Alisema kwamba, "Sasa tazama, najua ya kwamba hakuna Mungu duniani mwote, ila katika Israeli" (2 Wafalme 5:15). Aliahidi kutotumikia au kuabudu Mungu mwingine.

Yule msichana mdogo alikuwa mmisheni alipokuwa akitenda kazi. Ni lazima tufuate mfano wake na tuwe wamisheni kwa kuwaambia wengine yale ambayo Mungu anaweza kuwafanyia. Kuwaambia wengine habari njema kwamba Mungu anataka kuwaokoa watu wote inapaswa kuwa kazi tunayofanya kwa furaha.

## Mmisheni Katika Agano Jipya

Tulisoma katika somo lililopita kwamba Roho Mtakatifu aliwaongoza kanisa kuwatuma wamisheni (Matendo 13:1-3). Saulo, ambaye baadaye aliitwa Paulo, alifundishwa na waalimu bora zaidi wa dini. Hakumwamini Yesu akiwa kijana. Huduma yake ilikuwa kuwatesa wale waliokuwa Wakristo.

Mungu alikuwa na mipango maalum kwa Paulo. Mungu alimwambia mmojawapo wa watumishi wake waaminifu, "Huyu ni

chombo kiteule kwangu, alichukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli" (Matendo 9:15). Je, watu wa mataifa ni nani? Watu wa mataifa ni wale ambao si Wayahudi.

Paulo alifanya yale Mungu aliyomwambia afanye. Alitangaza jina la Mungu kwa mataifa pia (Matendo 13:47-49) na kwa Wayahudi wenzake wa Israeli (Matendo 9:26-30). Pia alieleza wafalme ujumbe huu. Moja ya shuhuda kuu zaidi katika Biblia ni ule wa Paulo akimshuhudia mfalme Agripa. Tusome Matendo 26:1-4, 22-23 na 28-29.

## Yesu Mmisheni

Yesu alikuja ulimwenguni akiwa na umisheni au kazi ya kutangaza upendo wa Mungu na wokovu wake. Malaika alisema katika Mathayo 1:21 "Nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."

Yesu alitumia muda wake ulimwenguni kuhubiri, kufundisha na kuponya. Alifanya haya ili kuwasaidia watu wengine kumjua Mungu. Yesu alitaraji watumishi wake watawaeleza wengine yale waliyokuwa wamejifunza kutoka kwake. Baada ya kuponywa, mtu mmoja alimwomba Yesu amruhusu akae naye (Yesu). Yesu alimtuma akamwambia, "Rudi nyumbani kwako, ukahubiri yalivyo makuu Mungu aliyokutendea" (Luka 8:39).

Yesu alifundisha wafuasi wake jinsi ya kufanya umisheni wao. Aliwaambia katika Yohana 3:11, "Lile tulijualo twalinena, na lile tuliloliona twalishuhudia." Baadae Yesu alizungumza na Nikodema yale aliyojua kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu. Soma Yohana 3:16-17. Tutazame mambo mengine ambayo Yesu aliwaambia wafuasi wake jinsi ya kuwa mashahidi wa Mungu. (Chagua wanawake tofauti wasome vifungu vinavyofuata halafu wajibu maswali au wajaze sehemu zilizoachwa wazi.

- Mathayo 5:14-16: Watu wengine watampa nani sifa na utukufu wakiona matendo yetu mazuri?
- Yohana 3:19-21: "Bali yeye aitendaye kweli huja kwenye nuru, ili matendo yake yaonekane wazi ya kuwa yametendwa katika ________________."
- Mathayo 28:19-20: Yesu aliwaambia wafuasi wake wawafanye watu wa ________________ yote kuwa wanafunzi wake.
- Matendo 1:8: Sisi ni mashahidi wa nani? Tunastahili kushuhudia wapi?

## Agizo Kuu

Tusome Mathayo 28:18-20 tena. Vifungu hivi vinaitwa Agizo Kuu. Agizo ni wakati mtu mmoja anapomwambia mwingine kufanya kazi au umisheni kwa niaba yake. Yesu hakuwaulize wafuasi wake ikiwa walitaka kufanya mambo haya. Alisema, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani." Halafu aliwaamuru au kuwaambia waende wakawafanye wengine kuwa wanafunzi.

Tukimpenda tutazitii amri zake. Tutapelekea ulimwengu uliopotea ujumbe wa upendo na wokovu. Tutawaambia waliopotea ya kuwa watu wote wamefanya dhambi, lakini Mungu anawapenda. Tutawaambia mpango wa Mungu wa wokovu. Tutawasaidia kuelewa kuwa hakuna huruma au msamaha wa dhambi mahali pengine popote ila kwa Kristo.

Soma maneno ya Yesu katika Yohana 14:21-24. Alisema kuwa alijua waliompenda kati ya wanafunzi wake. Yesu aliahidi kamwe hatatuwacha hali ya upweke katika huduma yetu. Aliahidi kuwa Roho Mtakatifu angewafariji na kuwasaidia wanaomtii. Je, unakumbuka kifungu cha mwisho katika Agizo Kuu? Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Mimi nipo pamoja nanyi sikuzote."

## Wamisheni Siku Hizi

Watu wengi hufikiri kuwa wamisheni ni watu wanaotoka kwao na kwenda sehemu nyingine kueleza watu habari za Kristo. Mwanamke mmoja ambaye ni mmisheni mbali na nyumbani kwake alisema, "Sikufanyika mmisheni nilipoitikia mwito wa Mungu na kwenda nchi ya kigeni. Nilifanyika mmisheni nilipofanyika Mkristo. Tunapomkubali Kristo kama Mwokozi, pia tunakubali umisheni au kazi ya kuwaeleza wengine habari za wokovu."

Soma Mathayo 9:35-38. Fikiri juu ya watu wote unaowaona kila siku. Je, wote wanamjua Yesu Kristo kama Mwokozi? Je, Yesu anawajali na kuwahurumia watu hawa? Ni kazi ya nani kueleza jamaa na majirani upendo wa Mungu na wokovu wake? Je, ungependa kuomba na kumuuliza Mungu akutumie kama mfanyi kazi wake?

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku:1)** 1 Mambo ya Nyakati 13:1-8; 16:1-2,
**Siku 2)** 2 Wafalme 5:1-18; **Siku 3)** Isaya 53;
**Siku 4)** Yohana 3:1-21; **Siku 5)** Yohana 3:22-36;
**Siku 6)** Matendo 9:1-31; **Siku 7)** Matendo 26

Somo la Tisa

# *NITATOA USHUHUDA WANGU VIPI?*

**Maandiko ya Biblia:** Wakolosai 4:1-6; 1 Yohana 2:1-6

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kama kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu." 2 Wakorintho 5:20

Kila mmoja wetu anapenda habari njema. Habari njema ni hii kuwa "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16). Kuhusu wokovu wako, ni nani aliyekueleza habari njema ya wokovu? (Wape muda wa kujibu.)

Je, kila mmoja katika jamaa yako amemwamini Yesu Kristo? Je, rafiki zako wote ni Wakristo? Je, yule anayekuuzia sukari au mboga? Je, huyo jirani yako mgeni? Je, watu hawa wote wanajua kuwa una habari yako njema? Je, unajua jinsi ya kuwaambia zawadi ya upendo wa Mungu na wokovu. Tutajifunza leo jinsi ya kushuhudia na kushiriki na wengine wapotevu habari njema.

## Mabalozi wa Kristo

Nchi yetu hutuma mabalozi katika nchi zingine. Mabalozi hawa huwakilisha matakwa ya nchi yetu. Wanawasaidia watu wa nchi zingine kuelewa nchi yetu. Soma kifungu cha kukariri. Biblia inasema, "kama kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu." Ikiwa wewe ni Mkristo, wewe ni balozi wa Kristo."

Watu wengi ambao si Wakristo hawaendi kanisani, wala hawasomi Biblia. Lakini katika nchi yetu wanawaona watu kila siku wakienda kanisani na kusoma Biblia. Wanajifunza habari za Yesu kwa kututazama wewe na mimi tulio mabalozi.

Katika somo lililotangulia tulijifunza kuwa Yesu anawajua wale wanaompenda. Alisema, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu" (Yohana 14:15). Soma 1 Yohana 2:1-6. Matendo yetu yanamwonyesha Yesu kuwa tunampenda. Pia matendo yetu yanawaonyesha wengine kuwa tunampenda na kuwa tu wafuasi wake. Biblia ilisema Wakristo "imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda."

Paulo aliandika katika barua yake kwa Wakristo wa mji wa Kolosai, alisema, "Muwe na hekima katika uhusiano wenu na watu wasioamini, mkitumia vizuri kila nafasi mliyo nayo" (Wakolosai 4:5,

Kisasa). Wale wasiomwamini Kristo huangalia maisha ya wale wanaomwamini. Itakuwa rahisi kwao kuamini tunayowaambia ikiwa wataiona tabia ya Kristo maishani mwetu. Watakuwa na hamu ya kupata habari njema tuliyo nayo.

## Uenezaji Injili Katika Nyakati za Agano Jipya

Soma 1 Petro 3:15. Wakristo ni sharti wawe tayari kuwatangazia wengine ujumbe wa Yesu Kristo. Je, tunawezaje kufanya jambo hili? Tuangalie jinsi watu watatu walivyo tangaza habari njema katika Agano Jipya.

Andrea alianza kutangaza habari njema mara tu baada ya kuwa mfuasi wa Yesu Kristo. Soma Yohana 1:35-42. Bila kupoteza wakati Andrea aliendа kumtafuta ndugu yake. Hakutumia maneno mengi au makubwa kutangaza habari njema. Kwa njia rahisi, Andrea alimweleza ndugu yake mabadiliko yaliyotendeka katika maisha yake. Halafu akamsaidia nduguye kujifunza zaidi kumhusu Yesu.

Katika somo lililopita tulisoma jinsi Paulo alivyomshuhudia mfalme. Kwanza alieleza juu ya maisha yake kabla ya kukutana na Yesu. Halafu akaeleza jinsi alivyomwamini na kubadilishwa maisha yake. Baadaye alimweleza mfalme jinsi naye anavyoweza kuwa mfuasi wa Kristo. Soma Matendo 26:22-29.

Mungu alimkutanisha Filipo na mgeni kutoka nchi tofauti aliyekuwa akisoma maandiko ya Agano la Kale. Mtu huyu alimwomba Filipo amsaidie kuelewa aliyokuwa akisoma. Filipo alikuwa amejifunza Agano la Kale na alielewa jisi ya kumweleza mtu asiyeamini. Matendo 8:35 inasema, "akianzia kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu." Mtu huyo akawa muumini siku hiyo!

## Uenezaji wa Injili ya Kristo Siku Hizi

Watu hawa kila mmoja alieleza habari yake njema kwa njia yake mwenyewe. Paulo alitumia maneno ya Kristo katika ushuhuda wake naye Filipo alieleza maana ya vifungu vya Maandiko. Tunaweza kufanya vivyo hivyo. Ebu tazama tena Somo la Kwanza. Jifunze jinsi ya kuwaeleza wengine somo hili. Kariri vifungu vilivyo katika *Mpango wa Wokovu* mwisho wa kitabu hiki. Halafu utakuwa tayari siku zote kuwaeleza wengine jinsi Yesu alivyobadilisha maisha yako.

Baadhi ya watu huogopa kushuhudia. Omba na kumuuliza Mungu akuongoze kama alivyomwongoza Filipo. Halafu jitayarishe na kumtegemea Mungu. Ukiona ni vema unaweza kuandika ushuhuda

wako. Unaweza kufanya mazoezi ya kutoa ushuhuda wako katika kikundi cha wanawake.

Tumia ushuhuda wa Paulo kama mwongozo. Simulia habari ya maisha yako kabla ya kuwa Mkristo. Eleza jinsi ulivyofanyika muumini. Eleza mabadiliko yaliyoko katika maisha yako. Tumia Biblia kueleza jinsi mtu anavyoweza kupata kipawa cha Mungu cha uzima wa milele kwa kumkubali Yesu Kristo.

## Biblia – Mwongozo Wetu

Biblia ni Neno la Mungu na kitabu chetu cha mwongozo. Ni kitabu cha kutueleza juu ya upendo wa Mungu. Soma 1 Wathesalonike 2:13 na Waebrania 4:12. Kuna wakati wa kutumia ushuhuda tulioandika au kupanga. Mara nyingi sana tutapata wakati wa kushuhudia tukisikiliza watu wakieleza matatizo yao na kuuliza maswali. Wakati huu tunapaswa kujua jinsi ya kuwapa jibu litokalo kwa Mungu.

Mungu hawezi kutuongoza kutumia maneno yake ikiwa hatuyajui na kuyaelewa. Tunapaswa kusoma na kujifunza Biblia kila siku. Tunapaswa kuhudhuria masomo ya Biblia kila juma. Tunapaswa kukariri vifungu vya Biblia. Tunapaswa kusikiliza Neno likihubiriwa katika ibada zetu. Baada ya kufanya hivyo tutakuwa tayari kufanya kazi yetu au kuwa wamisheni kwa kuwaeleza wengine ujumbe wa Mungu.

## Kanisa – Msaada Wetu

Unapoeleza habari njema utaulizwa maswali usiyoweza kujibu. Wakati mwingine watu hawatasikiliza ujumbe wetu au yale tunayowaeleza. Usiruhusu hali hii ikuzuie kuendelea kushuhudia. Tafuta msaada katika kanisa lako. Mwulize muhubiri wako au Mkristo mwenzako akusaidie kujibu maswali haya. Waulize wenzako katika kanisa kujibu maswali. Waulize wengine katika kanisa lako wawaombee wale wanaokataa ujumbe wa Mungu.

Je, Andrea alifanya nini baada ya kumwambia nduguye juu ya Yesu? Alimpeleka mahali ambapo angepata mafundisho zaidi. Kazi yetu ya umisheni ni kushuhudia na kuwasaidia Wakristo wapya kukua. Hatustahili kufanya mambo haya peke yetu. Tuwashirikishe wengine walio katika kanisa. Njia moja ya kushuhudia ni kuwahimiza watu wahudhurie masomo ya Biblia Jumapili na ibada pamoja na sisi.

Siku zote waulize waumini wapya wahudhurie ibada za kanisa pamoja na wewe. Pia unaweza kuwasaidia wapate mahali pa kuhudhuria ibada karibu na nyumbani kwao. Wakristo wapya wanahitaji jamaa ya kanisa iwatie moyo, iwafundishe na kuwasaidia.

Soma Waebrania 10:24-25. Jamaa ya kanisa inayohimiza na kusaidia huwa na nguvu katika kueleza wale wasioamini habari njema.

## Maombi – Hatua Yetu ya Kwanza

Ikiwa tunataka kufanya kazi yetu ya kumtangaza Kristo, ni sharti tuombe. Tunapaswa kujua kuwa hatuwezi kumwokoa mtu yeyote. Ni Mungu pekee awezaye kufanya hivyo, lakini anaweza kutusaidia kuwa wasaidizi wake. Paulo alitupatia misaada mingi mizuri ya jinsi ya kushuhudia. Walitufunidisha pia kuombea kupata nafasi ya kushuhudia. Soma Wakolosai 4:2-6.

Tunapaswa kumwomba Mungu atuongoze kufikia milango atakayo fungua. Je, kuna njia nyingine unayoweza kutumia ili kushuhudia? Je, unaweza kuanza masomo ya Biblia katika nyumba yako? Baadhi ya watu wasiowaamini wanaweza kuhudhuria masomo ya Biblia nje au mbali na jengo la kanisa. Je, unawezaje kuwashuhudia watu mahali ufanyapo kazi? Je, inawezekana watu wazungumze na wewe habari za Kristo ikiwa watakuona ukisoma Biblia wakati wako wa mapumziko kazini? Ungesema nini kuhusu watoto wanaocheza mpira wa miguu nje ya nyumba yako bila mpira wenyewe? Je, unaweza kuwanunulia mpira na kuwatazama wanapocheza? Labda baada ya mchezo wanaweza kusikiliza hadithi rahisi ya Biblia.

Pia tunaweza kuomba ili matendo yetu kila siku yawe ushuhuda kila siku. Je, wenzako wanakuona ukifuata amri za Yesu? Je, wanakuona ukiishi maisha kama Kristo alivyoishi? Je, wanakuona ukipenda jamaa yako na majirani kama ujipendavyo? Je, wanakuona ukieneza upendo wa Kristo bila uoga?

Soma Matendo 5:42. Mwombe Mungu akusaidie uwe na hamu zaidi ya kuwaambia wengine habari jema. Mwombe Mungu akufunulie jinsi awezavyo kukutumia kushuhudia. Omba ili uwe shahidi shupavu wa upendo na wokovu wa Mungu. Omba ili upewe maneno yaliyosahihi unapowaeleza wengine juu ya mambo ya imani. Mwombe Mungu akuongoze umshuhudie mtu juma hili.

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**

Kila siku juma hili jifunze *Mpango wa Wokovu* ulioko mwisho wa kitabu hiki. Anza kujifunza kwa moyo vifungu vya Biblia vilivyotumiwa. Mfikirie rafiki ambaye si Mkristo. Andika maneno ambayo utatumia kumwelezea mpango wa Mungu wa wokovu.

Somo la Kumi

# *JE! UKO TAYARI KUSHUHUDIA?*

**Maandiko ya Biblia:** 1 Wakorintho 2:1-5

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Mwe tayari sikuzote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu."* 1 Petro 3:15

Katika somo letu lililopita tulijifunza kuwa baadhi ya Wakristo huogopa kushuhudia. Wengine huamini kuwa hawana ufahamu wa kutosha kuweza kushuhudia mtu. Wengine hawashuhudii kwa kuwa huamini wenzao wanashuhudia vizuri zaidi kuwashinda. Wengine wanaweza kujisikia kuwa hawastahili kushuhudia kwa kuwa si kazi yao. *Kila Mkristo anapaswa kushuhudia.*

Je, unajua kuwa hata Paulo wakati mwingine aliogopa na kujisikia mdhaifu? Soma 1 Wakorintho 2:1-5. Hakutumia uoga na udhaifu wake kama sababu ya kukosa kushuhudia. Alijua kuwa mambo haya yalifanya ushuhuda wake kuwa na nguvu zaidi. Watu walielewa kuwa hawakuokolewa na maneno ya Paulo bali na uwezo wa Mungu.

Njia nyingine ya kushinda uoga wetu ni kwa kuwatazama wenzetu wakishuhudia. Msikilize mwanamke Mkristo anapomshuhudia jirani yake mgeni.

## Esta Anaeleza Habari Njema

(Waulize kina mama wawili waigize igizo hili. Esta anastahili awe na Biblia.)

**Esta:** (Anabisha hodi.) Bi. Yohana, hujambo?

**Maria:** Sijambo. Je, uhali gani?

**Esta:** Sijambo. Jina langu ni Esta Juma. Ninaishi katika ile nyumba iliyo nyuma ya duka la nyama.

**Maria:** Kumbe, ndio sababu nilikuona jana katika duka hilo. Ingia ukae kitini. Nashukuru umekuja. Jina langu ni Maria wa Yohana. Wewe ndiwe mgeni wangu wa kwanza. Subiri nikuletee chai.

**Esta:** La, usijali nimekunywa tayari. Mwenye duka la nyama aliniambia kuwa ulihamia kijiji hiki juma lililopita. Je, umemaliza kupanga vyombo vyote?

**Maria:** Ndio, watoto wangu na dada yangu walinisaidia.

**Esta:** Je, una watoto wangapi?

**Maria:** Nina watoto watatu. Mtoto wangu wa kiume ana miaka minane na mwingine miaka sita. Mtoto wangu mdogo ametoka nje na dada yangu.

**Esta:** Mimi pia nina watatu. Binti zangu wana miaka kumi na miwili na mwenzake kumi. Nina mtoto mvulana mwenye miaka minane. Bila shaka mtoto wako ndiye mvulana mgeni katika darasa hilo. Je, umeonana na mtu mwingine yeyote katika kijiji chetu?

**Maria:** La, nimekuwa na shughuli nyingi sana.

**Esta:** Kikundi chetu cha wanawake Wabatisti kitakutana kanisani kesho alasiri. Unaweza kuonana na wengi wa jirani zetu hapo. Je, mahali uliposhi mwanzo ulihudhuria kanisa gani?

**Maria:** Nilipoishi hapakuwa na kanisa karibu.

**Esta:** Maria, je, wewe ni Mkristo?

**Maria:** Ukweli ni kwamba mara nyingi wazazi walitupeleka kanisani.

**Esta:** Ni vizuri sana kuwapeleka watoto wetu kanisani. Je, umeamua Yesu Kristo awe Mwokozi wako? Je, umempa moyo wako?

**Maria:** Ninaelewa habari za Yesu, lakini sijaelewa swali lako. Ni nini maana ya Mwokozi?

**Esta:** Mimi ni Mkristo na Yesu ni Mwokozi wangu. Ameniokoa na nina uzima wa milele na baada ya maisha haya nitaendelea kuishi milele mbinguni. Je, ulipokuwa mtoto mdogo ulisikia hadithi ya Adamu na Hawa?

**Maria:** Ndio, hao walikuwa watu wa kwanza. Mungu aliwafanya waondoke mahali fulani kwa kuwa walikosa.

**Esta:** Ndio, hivyo ndivyo Biblia inavyotuambia. Biblia husema kuwa watu wote wametenda dhambi. Hali hii inatuzuia kuwa karibu na Mungu. (Soma Warumi 3:23.) Kifungu kingine, Warumi 6:23 kinasema, "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." Kwa sababu ya dhambi zetu tutakufa siku moja na tutaendelea kutengwa na Mungu. Mungu hapendelei hali hii. Anataka kutupa zawadi ya uzima wa milele ulio katika Mwanawe, Yesu.

**Maria:** Zawadi? Sijaelewa bado.

**Esta:** Hebu nisome Yohana 3:16. (Soma.) Mungu anatupenda na anatupatia njia ya kuweza kuwa pamoja naye. Nayo ni zawadi yake ya uzima wa milele. Atakuwa pamoja nasi tukiwa bado tunaishi

duniani. Tutakapo kufu tutaenda kuishi pamoja naye mbinguni. Hatuwezi kupata zawadi hii kwa kuifanyia kazi. Ni lazima tumwamini Yesu Kristo ndipo tupate zawadi hii.

**Maria:** Ninaamini kwamba kulikuwepo na mtu aliyeitwa Yesu. Lakini ulisema, "Mungu alimtoa Mwanawe." Je, una maanisha nini?

**Esta:** Tutazame tena Yohana 3:16. (Soma kifungu hiki.) Mungu alimruhusu Yesu aje ulimwenguni. Aliwekwa msalabani na akafa kwa ajili ya dhambi zetu. Baadaye Yesu alizikwa lakini alifufuka baada ya siku tatu. Alirudi mbinguni kuishi na Baba yake. Yuko huko sasa na anatungoja. Je, unaamini kuwa alikufa ili upate msamaha wa dhambi zako?

**Maria:** Ninaelewa yale unayosema. Lakini, tutapataje uzima wa milele?

**Esta:** Tusome 1 Yohana 1:9. (Soma kifungu hiki.) Tunapaswa kukiri au kukubali kuwa tu watenda dhambi na kuwa hatumtii Mungu. Tunapaswa kuhuzunikia dhambi zetu na kumuuliza Mungu atusamehe. Pia ni sharti tumwombe Mungu atawale maisha yetu na awe nasi kila siku.

**Maria:** Je, anaweza kunisamehe? Mimi sina wema wa kutosha hata nimwombe anisamehe. Je, itakuwaje nikitenda dhambi tena baada ya kusamehewa?

**Esta:** Hatutakuwa wakamilifu bila dhambi baada ya kuwa Wakristo. Mungu atatusaidia na kutupa nguvu tutakapojaribiwa kutenda maovu. Umeuliza ikiwa Mungu anaweza kukusamehe. Tusome Warumi 10:9-10. Ni nini unachoamini moyoni? Je, unafurahia maisha yako? Je, unataka kumwuliza Yesu aingie katika maisha yako?

**Maria:** Nina mambo mengi ambayo sielewi.

**Esta:** Hiyo ndiyo sababu Wakristo hujifunza Biblia, Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu tunakutana na kanisa ili kuomba, kuabudu na kujifunza zaidi jinsi ya kumtumikia Mungu. Hakuna mtu yeyote anayejua mambo yote. Lakini tutajifunza mambo zaidi tukimruhusu Mungu atawale maisha yetu.

**Maria:** Kuna jambo lingine moja. Je, kanisa lako ni lile linalobatiza mtoni? Mimi sijui kuogelea na maji huniogopesha sana.

**Esta:** Ndio. Wabatisti hukushauri ubatizwe. Kwa tendo hili huwa unaonyesha ulimwengu kuwa umemuomba Mungu akusamehe dhambi na kukusaidia kuwa mtu mpya. Unapomkubali Yesu kuwa Mwokozi,

unastahili kwenda na kujulisha kanisa. Kanisa letu litakusaidia kuelewa maana ya ubatizo na njia zingine za kumfuata Kristo. Je, uko tayari kupokea kipawa cha Mungu cha uzima wa milele? Je, unataka tuombe pamoja na umkubali Yesu awe Mwokozi wako?

**Maria:** Ndio.

**Esta:** Maria, omba kwa kurudia maneno haya nyuma yangu. (Esta anaomba fungu moja la maneno naye Maria anayarudia.) "Bwana Yesu, ninakuhitaji. . .Nasikitikia dhambi zangu. . .Nakuomba uje na uishi ndani ya moyo wangu na maisha yangu. . .Asante kwa kufa ili nipate uzima wa milele. . .Asante kwa kunisamehe dhambi zangu. Amen."

**Maria:** Nataka niende na wewe katika mkutano wenu kesho. Je, naweza pia kwenda nawe kanisani Jumapili?

**Esta:** Ndio, sasa wewe ni jirani yangu mpya, na dada yangu katika Kristo.

**Kiongozi:** Watu fulani huwa tayari na wao hutaka tu uwashuhudie kidogo. Wengine wanaweza kukuuliza maswali mengi na baadaye wanakubali kuwa Wakristo. Wengine watasikiliza mpango wa wokovu mara kadhaa kabla ya kuamini. Wako wengine ambao kamwe kabisa hawataamini nao wengine hawatakuruhusu uwashuhudie. Tunapaswa kukumbuka kuwa sio sisi tunaookoa mtu. *Wokovu ni kazi ya Mungu! Kazi yetu ni kueleza habari njema.*

Waulizwe washiriki wa kikundi chako waeleze jinsi walivyofanyika Wakristo. Waulize kina mama waeleze ni mara ngapi wameenda kushuhudia.

Tusome Warumi 10:14-15. Je, inawezekana kuwe na mtu ambaye hajasikia habari njema kwa kuwa hujamwambia? Fikiri juu ya mtu mmoja utakayemweleza habari njema juma hili. Je, kanisa lako linamlipa mchungaji mshahara ili aweze kutumia wakati wake kuhubiri na kushuhudia? Je, inawezekana kanisa lako limtume mtu sehemu nyingine aeleze habari njema? Tukome hapa kwa sasa ili tuombee mambo haya.

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** Yohana 4:7-42; **Siku 2)** Yohana 5:16-47;
**Siku 3)** Matendo 4:1-21; **Siku 4)** Matendo 10:23-48;
**Siku 5)** Matendo 16:25-34; **Siku 6)** Matendo 16:11-15; 18:24-28;
**Siku 7)** Warumi 10:1-13; Waefeso 2:1-10

Somo la Kumi na Moja

# *JE, UWW/WMU NI NINI?*

**Maandiko ya Biblia:** Mathayo 28:19-20, 1 Wakorintho 3:7-4:2

**Kifungu cha Kukumbuka:** *'Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu."* 1 Wakorintho 3:9

Makanisa ya kwanza ya Wabatisti Afrika ya Mashariki yaliundwa 1959. Wanawake katika makanisa hayo walikuwa kama wanawake walio katika makanisa ya leo. Walitaka wakue katika maisha ya Kikristo na kutii amri za Yesu. Walihitaji kuomba na kujifunza Biblia wakiwa na wanawake wenzao Wakristo. Wanawake walianza kukutana pamoja ili kutimiza mahitaji haya.

Kadiri miaka ilivyoendelea ndivyo nayo kazi ya Wabatisti katika Afrika ya Mashariki ilivyoendelea kukua. Kazi ya wanawake imekuwa sehemu muhimu katika kuikuza kazi hii. Hivi sasa, muungano huu unaitwa ***Ushirika Wa Wanawake Waenezao Injili (UWW au Ushirika)*** au ***Woman's Missionary Union (WMU).***

Katika *Ushirika* tunajifunza Biblia na kujifunza jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo. Tunajifunza juu ya uwakili, maombi na kushuhudia. Tunawafundisha wanawake vijana na wasichana katika kanisa letu. Pia tunajifunza kuhusu kazi ya Wakristo wa nchi zingine na mahitaji ya watu wao.

*Ushirika* pia hutoa nafasi ya wanawake kufanya mazoezi ya mambo wanayojifunza. Katika mkutano wetu huomba pamoja. Tunatoa sadaka ya kusaidia kazi ya kueneza Injili. Sisi wanawake Wakristo pia tunatoka nje kushuhudia na kutimiza mahitaji ya wale wanaotuzunguka.

## Wimbo Wetu

Wimbo wa *Ushirika* ni **Nataka Nimjue** (181, *Nyimbo za Imani Yetu* na 159, *Nyimbo za Sifa*). Sikilizeni nitakaposomo maneno ya wimbo huu. (Soma wimbo huu.) Tuimbe wimbo huu pamoja.

*NATAKA NIMJUE*

*Nataka nimjue Yesu, na nizidi kumfahamu,*
*Nijue pendo lake, na wokovu wake kamili.*
*Zaidi, zaidi, nimfahamu Yesu,*
*Nijue pendo lake na, wokovu wake kamili.*

## Kifungu Chetu

Kifungu chetu cha Ushirika wa Wanawake ni *"Sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu" (1 Wakorintho 3:9)*.

Kila Mkristo ametumwa kueneza upendo wa Mungu na wokovu wake kwa wasiomjua. Tuna umisheni huu au kazi hii kwa kuwa kila mmoja wetu alifanyika mtoto wa Mungu tulipomfanya Kristo kuwa Mwokozi wetu. Tunapaswa kufanya kazi ya Baba yetu. Tunawahusisha watoto wengine wa Mungu katika umisheni wa Mungu. Sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu akiwa kiongozi wetu.

Mtenda kazi mzuri hujua jinsi ya kutenda kazi yake. Ikiwa tunataka kuwa viongozi wa Mungu na wenye nguvu tunapaswa kuwa Wakristo waliokomaa. Tunapaswa kujifunza Biblia, kuomba na kujifunza yote tunayoweza kujifunza ili kumtumikia yeye.

## Alama Yetu




Hapa kuna picha ya alama yetu. Ni mfano wa vichwa viwili vya samaki iliyotumiwa na Wakristo wa mwanzo. Mfano huu ulitumika kwa sababu katika lugha ya kiyunani herufi za kwanza za "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Mwokozi" zikiunganishwa huwa ni neno "samaki." Wengi wa Wakristo wa mwanzo waliteswa. Muumini angechora samaki kuwajulisha wenzake kwa siri kuwa yeye ni mfuasi wa Kristo.

Alama hii inazungukwa na maneno haya "Umoja wa Wanawake, Makanisa ya Wabatisti" ambalo ni jina la umoja wetu. Alama hii hutumiwa na wanawake katika nchi nyingi za ulimwengu, maneno hayo yakiwa katika lugha yao.

Kuna Biblia iliyofunguliwa ambayo ina kifungu chetu katikati ya alama. Juu ya Biblia kuna mwenge unaowaka ambayo ni mfano wa Mwokozi wetu ambaye ni *Nuru ya Ulimwengu* (Yohana 8:12). Mwenge huu uko nyuma ya ulimwengu kuonyesha kuwa Mungu siku zote yuko karibu kututia nguvu na kutuokoa. Alama ya ulimwengu huonyesha kuwa tumweleze kila mmoja ulimwenguni ujumbe wa Mungu.

## Kusudi Letu

*Ushirika* ni chama cha wanawake ambao ni "Wafanya kazi pamoja na Mungu." Lengo letu ni kutangaza ujumbe wa wokovu; kusisitiza umuhimu wa maisha ya Kikristo nyumbani na katika jamii; kujifunza Biblia; kuomba kwa mtu binafsi na kuomba katika jamaa mbalimbali; kutoa zaka na sadaka zetu; kuwatumikia wengine; na kueneza Injili kote Afrika Mashariki na ulimwenguni kote.

## Mikutano Yetu Na Viongozi Wetu

Wanawake katika makanisa mengi ya Kibatisti hukutana mara moja kila juma. Wanachagua siku na wakati unaofaa kwao. Katika mikutano yao wanaimba na wanashirikisha wenzao kuhusu kufaulu au kushindwa kwao na jinsi ya kutatua matatizo yao. Wanawake wanaomba na kujifunza Biblia pamoja.

Wanawake Wabatisti, katika mikutano yao hupanga mipango ya kukidhi mahitaji ya kanisa na jamii yao. Wanawaeleza wenzao mambo waliyojifunza katika kusaidia na kuwashuhudia watu. Wao huwa kama watenda kazi wa Mungu.

Kila kikundi cha *Ushirika* huchagua viongozi wao kila mwaka ili wawaongoze katika kazi na mikutano. Viongozi hawa ni: mwenye kiti, mwenye kiti mdogo au nwenye kiti wa mpango, mwandishi na mweka hazina. Waulize viongozi wa Umoja wa Wanawake katika jumuiya yako ndogo ili wakusaidie kuanza kikundi chako na kuchagua viongozi wa kwanza.

## Vitabu Vyetu

Mipango ya mikutano yetu imo katika kitabu kiitwacho **Iwe Nuru**. Viko vitabu vingi vya **Iwe Nuru** na vingine vipya huandikwa kila mwaka. Vitabu hivi vimechapwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili na vina masomo kumi na mbili. Kila mshiriki aliye katika kikundi chako anahitaji nakala moja ya **Iwe Nuru**.

Kila kiongozi anapaswa kuwa na nakala moja ya **Kitabu cha Maelezo**. Kitabu hiki hueleza maana ya Ushirika wa Wanawake. Pia kinaeleza kazi ya kila kiongozi. Kila chama cha *Ushirika* wanahitaji **Kitabu cha Repoti.** Kitabu hiki huwasaidia kuweka taarifa mbalimbali kuhusu kikundi chenu.

Viongozi wenu katika jumuiya ndogo wanaweza kuwaeleza mnapoweza kununua vitabu hivi. Pia vitabu vinaweza kununuliwa katika:

> Kenya Baptist Media, P.O. Box 30370, Nairobi, Kenya *au*
> Baptist Literature Centre, S.L.P 1240, Moshi, Tanzania

## Sadaka Zetu

Yesu alitufundisha tuwapende jirani zetu na tuwatunze walio na mahitaji. Sadaka hukusanywa wakati wa mikutano yetu ili itumiwe kufanya kazi ya "wafanya kazi pamoja na Mungu." Vikundi vingi huendelea kuongeza matoleo yao kila wanapokutana.

Sadaka hii inaweza kutumika kwa mfano, kumsaidia mama wa makamu asiyeweza kulipa kodi ya nyumba kwa mwezi mmoja. Inaweza kununulia jamaa fulani dawa labda walio na watoto wengi wagonjwa. Sadaka hii si ya kulipa mshahara wa mchungaji au kutayarisha mlo maalum katika kikundi chetu. Inatolewa kutumika katika kutangaza upendo wa Mungu na wokovu kwa wale wasio Wakristo.

Je, wanawake wote katika kikundi chako wanaweza kununua kitabu cha **Iwe Nuru**? Ni vizuri ikiwa kila mwanamke atanunua kitabu chake. Baadhi ya wanawake hawawezi. Kikundi chako kinaweza kuwauliza wenye uwezo watoe sadaka zaidi ili wanunulie wasioweza wapatiwe vitabu hivi.

Katika somo lifuatalo tutajifunza jinsi kikundi chetu cha Ushirika kinavyohusiana na jumuiya ndogo na kikundi cha taifa cha Umoja wa Wanawake. Sisi ni sehemu moja ya vikundi vya Wabatisti ulimwenguni kote. Tukiwa sehemu moja ya vikundi hivi vikubwa tunaweza kuwa "wafanya kazi pamoja na Mungu" kwa njia ambazo tukiwa peke yetu hatuwezi. Hivi vikundi vikubwa ni lazima wapate msaada kutoka makanisa ya sehemu hiyo ili waweze kufanya kazi yao. Hii ni pamoja na kuwagawia sadaka yetu. Pia ina maana tutatoa wakati wetu na wakati mwingine tutatoa nguo na chakula kuwasaidia wenye mahitaji.

Mungu anataraji sadaka ya pesa zetu. Lakini kwanza tunapaswa tujitoe sisi wenyewe kwa Mungu. Soma 1 Wakorintho 4:1-2 na 2 Wakorintho 8:5.

Tuombe Mungu atusaidie kuwa watumishi waaminifu wa Mungu. Omba ili Mungu atusaidie tunapoanza *Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili* katika kanisa letu. Tuombe Mungu atusaidie siku zote ili tukue tukiwa "Wafanya kazi pamoja na Mungu."

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** 1 Wakorintho 3:1 - 4:5; **Siku 2)** Wagalatia 3:26 - 4:7;
**Siku 3)** Waefeso 6:10-20; **Siku 4)** Zaburi 27;
**Siku 5)** 1 Timotheo 4:6-16; **Siku 6)** 2 Wakorintho 4;
**Siku 7)** Zaburi 86:1-13

Somo la Kumi na Mbili

# *SHABAHA ZETU NI ZIPI?*

**Maandiko ya Biblia:** Wakolosai 1:3-14; 1 Timotheo 4:6-16

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halai neno la kweli."* 2 Timotheo 2:15

Kazi yetu na mafundisho ya Ushirika huongozwa na shabaha tano. Shabaha hizi ni kazi au matendo tunayopaswa kutenda tukiwa wanawake Wakristo. Tutajifunza mambo haya leo na jinsi tunavyopaswa kufanya ili kufikia shabaha hizi.

## SHABAHA YA KWANZA: Kupata Ufahamu

*Tutajaribu kuwa na ufahamu wa watu wote na kuwahurumia wale ambao wamepotea bila Kristo. Tutajaribu pia kuwa na ufahamu wa kazi yetu kama wanawake Wakristo. Tutaendelea kufanya mambo haya kwa kujifunza Biblia na kwa mafunzo yetu katika **Iwe Nuru** na vitabu vingine vya Kikristo.*

Soma Yohana 3:16-17 na Mathayo 28:19-20. Je, tunawezaje kueneza upendo wa Mungu na wokovu wake kwa ulimwengu wote? Je, twawezaje kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi? Tunapaswa kulijua Neno la Mungu. Zaburi 119:11 inasema, "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako." Tunapaswa kujua kuuelewa ulimwengu na watu waishio ndani yake. Tunapaswa kujifunza jinsi ya kuwaeleza wengine habari njema tuliyo nayo.

Ili tufikie shabaha yetu ya kwanza ni sharti tujifunze Biblia na **Iwe Nuru** katika mkutano wetu wa Ushirika. Tunapaswa kujifunza Biblia nyumbani na kuhudhuria mafundisho kanisani mwetu. Tunapaswa kuwatia moyo wanawake wote kanisani mwetu ili wajiunge na Ushirika. Viongozi wanapaswa kujifunza kazi zao ili wawe viongozi wema wa kazi ya Mungu.

Kila mwaka wanawake Wabatisti huwa na *Juma la Maombi* (Kenya ni mwezi wa sita na Tanzania mwezi wa saba). Pia tuna *Siku ya Maombi* Jumatatu ya kwanza mwezi wa kumi na moja kila mwaka. Huu huwa wakati wa kuungana na wanawake wengine ulimwenguni kote kuomba. Afisi ya kitaifa ya Umoja wa Wanawake hutusaidia kupokea mipango nyakati hizi za maombi. Mipango hii itatufundisha zaidi juu ya maombi. Mipango hii itatufundisha zaidi

juu ya mahitaji ya wenzetu ulimwenguni na kuwa mwongozo wetu wa maombi.

## SHABAHA YA PILI: Kukua Katika Maisha ya Kiroho

*Tutajaribu kutia nguvu maisha ya kiroho ya washiriki kwa kuwavuta kuomba na kusoma Biblia katika mikutano yetu, nyumbani, na katika maisha ya kila mmoja binafsi.*

Mara nyingi Paulo aliwatia moyo washiriki wa kanisa la kwanza kukua katika Ukristo wao. Soma Waefeso 4:14-15 na Wakolosai 1:9-14. Biblia, Neno la Mungu, ni mwongozo wetu wa jinsi ya kuishi na kukua katika Ukristo wetu. Pia Mungu hutuongoza katika maombi. Wakati wa maombi tunazungumza na Mungu na tunasikiliza maneno anayotuambia.

Mungu anahitaji viongozi wenye nguvu wafanye kazi yake. Tunaweza kuwa Wakristo shupavu na wanaokua ikiwa tutajifunza neno lake na kutenda yale tunayofundishwa. Hatupaswi tu kusoma Biblia katika mikutano yetu na kusoma somo la siku hiyo. Tunastahili kutafuta kile ambacho Mungu anaeleza. Tunastahili wakati wetu kuwa na sehemu ya maombi katika mikutano yetu ili tupate kuzungumza na Mungu. Siku zote tumsikilize yeye ili atuonyeshe tunavyoweza kumtumikia na kumtii.

Kila mwanamke anayetaka kukua katika Ukristo wake anapaswa kusoma na kujifunza Biblia kila siku. Anapaswa kutenga wakati kila siku kuzungumza na Baba yake. 1 Wathesalonike 5:17 inasema, "Ombeni bila kukoma." Tunapaswa pia kuwafundisha watoto wetu kujifunza Biblia na kuomba. Njia moja ya kufanya hivi ni kuwa na wakati wa jamaa kusoma Biblia na kuomba nyumbani kila siku.

## SHABAHA YA TATU: Kuwa Mashahidi Wakristo

*Tutajaribu kuwaongoza washiriki kuwa mashahidi Wakristo kwa ushuhuda wa Kristo kwa waliopotea na utumishi wa jamii inayoonyesha upendo wa Kristo. Tutajitahidi kutia nguvu maisha ya Kikristo nyumbani na kati ya jamii.*

Wokovu ni kipawa cha Mungu. Hatustahili kufanya matendo mema ili kupata kipawa hiki. Soma Waefeso 2:8-10 na Yakobo 2:14-18. Yakobo anatukumbusha kuwa mtu yeyote aliyeokoka atajaribu kumtii na kumtumikia Mungu, Baba yetu. Katika Ushirika kazi ya kushuhudia na kuhudumia wengine katika jina la Yesu Kristo huitwa *Utumishi wa Jamii.*

Matendo 1:8 husema, "Nanyi mtakuwa mashahidi wangu." Tunapaswa kutafuta jinsi ya kuwasaidia wengine jambo linaloonyesha upendo wa Mungu kwao. Kila mshiriki anapaswa kujitahidi kufanya kazi ya kumshuhudia Kristo kila siku. Ni lazima tupange wakati wa kuwashuhudia wale ambao hawajamjua Yesu kama Mwokozi wao. Tunapaswa kuwaeleza habari za kipawa cha Mungu cha wokovu.

Kikundi chetu kinastahili kupanga njia moja au zaidi za kuwatumikia wengine katika jina la Yesu na kushuhudia kila mwezi. Tuwahimize washiriki watafute njia kila siku kuwaonyesha wengine upendo wa Mungu kutangaza wokovu wake kwa waliopotea.

## SHABAHA YA NNE: Kushiriki Mali Yetu

*Tutajaribu kuendeleza Wakristo hushiriki kwa njia ya kufundisha uwakili. Tutawatia moyo washiriki kutoa fungu la kumi na kutoa sadaka maalum kupeleka neno la Mungu katika sehemu nyingine za nchi yetu na dunia.*

Yesu alisema, "Ni heri kutoa kuliko kupokea" (Matendo 20:35). Soma jinsi makanisa ya Makedonia yalivyofuata mafundisho haya katika 2 Wakorintho 8:1-8. Uwakili ni mtu kutoa wakati wake, vipawa, na pesa pamoja na maisha kwa jumla kumpa Yesu. Kila mwanamke anapaswa kujitahidi kuwa shahidi mwema wa vitu vyote ambavyo amepewa na Mungu. Hii ndiyo sehemu ya ushuhuda wetu kwa wenzetu. Kila mwanamke anapaswa kutoa sehemu moja ya kumi ya vyote alivyo navyo na kupeana kanisani kwa kazi ya Mungu. Mabaki yanapaswa kutumiwa kwa njia ya kumpendeza Mungu.

Katika Ushirika tuna sadaka aina mbili ya kusaidia kutangaza Injili. *Sadaka ya Juma la Maombi* hutumika katika nchi kueneza ujumbe wa upendo wa Mungu na wokovu. *Sadaka ya Siku ya Maombi* hutimiza mahitaji ya wanawake Afrika na katika sehemu nyingine za ulimwengu.

Sadaka zinazotolewa katika mikutano ya kila juma hutusaidia kutimiza shabaha zetu. Tutatumia sehemu moja ya sadaka zetu kutumika na kuwasaidia wengine katika jamii ya kanisa. Tutatoa sehemu ya sadaka yetu kwa jumuiya yetu ndogo na jumuiya kuu ya Umoja wa Wanawake. Pesa hizi zitasaidia mpango wa kazi ili tutimize shabaha zetu.

## SHABAHA YA TANO: Kufundisha Watoto na Vijana

*Tutajaribu kuwafundisha watoto wetu na wengine juu ya Mwokozi wetu. Tutajitahidi kuongoza watoto na vijana kufahamu habari ya Kristo na jinsi ya kueneza Injili katika vyama vinavyokutana katika makanisa yetu.*

Wakati mmoja Yesu aliulizwa ni amri ipi iliyo kuu au muhimu zaidi. Soma jibu lake katika Mathayo 22:37-40. Soma katika Mathayo 5:17-20 yale Yesu aliyowaambia wafuasi wake kuhusu kutii sheria za Agano la Kale. Amri ambayo Yesu alisema ni kubwa kuliko zote ilitolewa na Mungu akampa Musa katika Kumbukumbu la Torati 6:5. Soma Kumbukumbu la Torati 6:5-8. Ili tufikie shabaha yetu ya mwisho, tunapaswa kutenda kulingana na maneno ya Mungu katika vifungu hivi.

Tunapaswa kuwafundisha watoto wetu habari za Yesu. Pia tunapaswa kufundisha watoto wote wa kanisa letu na jirani zetu Neno la Mungu. Mithali 22:6 inasema, "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee."

Njia moja ya kuwafundisha na kuwalea watoto ni kwa kuanza vikundi vya wavulana na wasichana katika kanisa letu. Vikundi hivi huitwa **Wajumbe wa Yesu** (WY). Katika Wajumbe wa Yesu watoto hufundishwa mpango wa Mungu wa kuleta wokovu ulimwenguni. Wanafundishwa jinsi ya kuwaambia wengine habari njema za Yesu Kristo. Kuna mipango iliyopangwa kwa kusudi la kutumiwa katika vikundi hivi. Tunaweza kununua mipango hii kutoka Kenya Baptist Media au Baptist Literature Centre.

**Kiongozi:** Katika somo linalofuata tutajifunza jinsi ya kufanya kazi na wengine kunavyoweza kutusaidia kufikia malengo yetu. Pia, tutaomba na kumwuliza Mungu atuongoze tunapo mtumikia na kumtii kupitia kwa Ushirika wa Wanawake (UWW au WMU). Hebu tufunge somo hili kwa kusoma Wakolosai 1:3-6. Tuombe na tumwuliza Mungu atusaidie kuendelea kukua kama "*Wafanya kazi pamoja na Mungu.*" (Mkiwa na wakati, zungumzieni jinsi kundi lenu linaweza kutimiza malengo yenu na mumwombe Mungu awaongoze.)

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** 2 Timotheo 1; **Siku 2)** 2 Timotheo 2;
**Siku 3)** 2 Timotheo 3; **Siku 4)** 2 Timotheo 4;
**Siku 5)** Zaburi 63; **Siku 6)** 2 Wakorintho 8:1-15;
**Siku 7)** Warumi 15:1-13

Somo la Kumi na Tatu

# *WANAWAKE WABATISTI WANAUNGANA!*

**Maandiko ya Biblia:** Warumi 15:5-13

**Kifungu cha Kukumbuka:** *"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."* Wakolosai 3:17

Washiriki wa kanisa letu wanafanya kazi pamoja kama "wafanya kazi pamoja na Mungu." Pia sisi hufanya kazi pamoja na makanisa mengine katika sehemu yetu na ulimwenguni.

Biblia inatueleza njia ambazo kanisa la kwanza lilifanya kazi na makanisa mengine. Makanisa ya Makedonia walitoa sadaka ya kuwapa maskini huko Uyahudi (Warumi 15:26). Wakristo walipoondoka kutoka mji mmoja hadi mwingine waliwatafuta waumini wenzao (Matendo 16:13-15). Barua za Paulo zilitumwa kutoka kanisa moja hadi lingine na akawatumia salamu za upendo na kuwatia moyo Wakristo (Matendo 15:30-31). Makanisa ya kwanza yalituma wahubiri wawapelekee watu Neno la Mungu (Matendo 13:1-3).

Makanisa ya Wabatisti huungana siku hizi kwa wingi wa njia zilizotajwa ili kusaidiana. Wanaombeana, wanafundishana, na kusaidiana. Makanisa ya Wabatisti wanashirikiana. Wakati mwingine wanaungana ili kushuhudia, kuhubiri, na kutuma waijilisti.

Leo tutajifunza jinsi wanawake Wabatisti wanavyoungana kufanya kazi bora katika kumtumikia Bwana wao. Tutaona jinsi wanawake wetu wanavyoungana katika jumuiya yetu ndogo, katika taifa, katika bara la Afrika na mwisho katika ulimwengu mzima.

## Umoja wa Wanawake wa Jumuiya Ndogo

*Jumuiya ndogo* ni kikundi cha makanisa ya Wabatisti yaliyo mahali pamoja na kufanya kazi pamoja. *Ushirika* katika makanisa haya huungana na kuwa *Umoja wa Wanawake Waenezao Injili* wa jumuiya ndogo. Katika mikutano ya *Umoja* wa jumuiya ndogo, wanawake wa makanisa mbali mbali hujifunza, huomba na huwa na ushirika wao kwa wao. Wanashirikiana kazi zao na wenzao katika kikundi na kuhimizana.

Wanawake katika *Umoja* wa jumuiya ndogo hufanya kazi katika miradi ambayo kikundi cha kanisa moja hakiwezi kufanya. Mikutano ya *Umoja* wa jumuiya ndogo hupangwa kila mwaka ili kufundisha na kuhimiza wanawake. *Umoja* wa jumuiya ndogo hutoa mwongozo na kuwaimarisha na kutia moyo *Ushirika* mpya kwa kuwatuma viongozi waliokomaa kutembelea vikundi hivi. Tunatoa sehemu moja ya sadaka zetu na kuipa *Umoja* wa jumuiya ndogo ili kusaidia kulipia mambo haya. Tunawachagua viongozi vya Umoja wa jumuiya ndogo jinsi tunavyofanya kanisani mwetu.

## Umoja wa Wanawake wa Taifa

Makanisa ya Wabatisti katika taifa letu yaliyo na imani sawa na yetu huungana pamoja katika *jumuiya kuu*. Pia tuna idara ya *Umoja wa Wanawake* katika taifa letu. Katika *Umoja wa Wanawake* wa taifa letu tunaungana na wanawake wengine wengi walio *"wafanya kazi pamoja na Mungu."* Tikiwa washiriki katika kikundi hiki kikubwa na chenye nguvu tunashiriki kutangaza upendo na wokovu wa Mungu katika nchi na ulimwengu mzima.

*Umoja wa Wanawake* wa taifa letu hutusaidia kushiriki ujumbe wa Mungu katika eneo letu tunapo fundisha, tunapokutana na kukuza *Wajumbe wa Yesu.* Wanatupatia mbinu za kutusaidia kuanza na kuimarisha *Umoja wa Wanawake* na kazi yao katika nchi nzima. Hutupa mpango wa *Juma la Maombi* na *Siku ya Maombi.* Pia wanahakikisha kuwa vitabu vya mafundisho kama hiki vinapatikana ili tutumie.

## Ushirika Wa Wabatisti wa Ulimwengu

*Muungano wa Wabatisti wa Ulimwengu* (Baptist World Alliance) ni ushirika wa vikundi vya Wabatisti kutoka sehemu zote za ulimwengu. Mojawapo ya sehemu za Muungano wa Wabatisti wa Ulimwengu ni *Idara ya Wanawake. Idara ya Wanawake* imegawanywa katika bara kuu aina tano. Tunahusika na *Idara ya Wanawake* kwa njia ya uanachama wetu katika *Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Afrika.*

*Idara ya Wanawake* inasaidia wanawake Wabatisti kumtumikia Mungu wakiwa watenda kazi wake. Wanawasaidia wanawake kutoka sehemu zote za ulimwengu kuelewana wao kwa wao vizuri zaidi.

*Siku ya Maombi ya Wanawake Wabatisti wa Ulimwengu* hupangwa na Idara ya Wanawake. Jumatatu ya kwanza ya mwezi wa

kumi na moja tunaungana kwa maombi na wanawake ulimwenguni kote. Tunapojifunza mpango wa Siku ya Maombi kila mwaka, tunatambua mahitaji ya wanawake kutoka sehemu nyingine za ulimwengu. Tunajifunza jinsi ya kuwaombea. Sadaka ya Siku ya Maombi hutumiwa Afrika na ulimwenguni kote kuwasaidia wanawake kueneza upendo na wokovu wa Mungu.

## Mimi ni Sehemu ya Ushirika

Sisi ni wanawake Wabatisti wanaoamini kuwa *"Sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu."* Tutumie wakati huu sasa kumshukuru Mungu kwa kuwa Baba anayetupenda. Tumshukuru kwa ajili ya Mwanawe na wokovu wetu. Pia tutaomba na kumuuliza Mungu atuongoze sisi binafsi na *Ushirika* wanaotaka kuwa watenda kazi wake.

Tufanye hivi kwa kusoma vifungu katika Zaburi na kuomba msaada wa Mungu ili tufikie kila shabaha ya shabaha zetu. (Ikiwezekana, mwulize mwanamke tofauti asome na kuomba kwa kila moja ya mambo yafuatayo. Au unaweza kusoma vifungu na shabaha na umwulize mmoja aombe akifuata mapendekezo.)

- Soma Zaburi 86:6-13 na Shabaha ya Kwanza: *"Tutajaribu kuwa na ufahamu wa watu wote na kuwahurumia wale ambao wamepotea bila Kristo. Tutajaribu pia kuwa na ufahamu wa kazi yetu kama wanawake Wakristo. Tutaendelea kufanya mambo haya kwa kujifunza Biblia na kwa mafunzo yetu katika **Iwe Nuru** na vitabu vingine vya Kikristo."*

**Mwombe Mungu atusaidie kuelewa na kuwajali waliopotea katika nchi yetu na mataifa mengine. Mwombe Mungu atufundishe na kutuonyesha kazi anayotaka tufanye.**

- Soma Zaburi 51:1-10 na Shabaha ya Pili: *"Tutajaribu kutia nguvu maisha ya kiroho ya washiriki kwa kuwavuta kuomba na kusoma Biblia katika mikutano yetu, nyumbani, na katika maisha ya kila mmoja binafsi."*

**Omba kuwa kila mwanamke katika *Ushirika* wetu atakua akiwa na hekima ya Mungu. Waulize wanawake waombe kwa kusoma pamoja vifungu vifuatavyo. "Uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu" (Zaburi 51:10).**

- Soma Zaburi 96:1-4 na Shabaha ya Tatu: *"Tutajaribu kuwaongoza washiriki kuwa mashahidi Wakristo kwa ushuhuda wa Kristo kwa*

*waliopotea na utumishi wa jamii inayoonyesha upendo wa Kristo. Tutajitahidi kutia nguvu maisha ya Kikristo nyumbani na kati ya jamii."*

**Tuombe tuwe mashahidi shupavu wa Kristo kila siku. Tuombe ili Mungu atusaidie tuone njia za kufanya kazi pamoja naye katika jamii na kueneza upendo wake. Tuombe ili tupate njia za "Tangezeni wokovu wake siku kwa siku" na "Wahubirini mataifa habari za utukufu wake, na watu wote habari za maajabu yake."**

- Soma Zaburi 56:10-13 na Shabaha ya Nne: *Tutajaribu kuendeleza Wakristo kushiriki kwa njia ya kufundisha uwakili. Tutawatia moyo washiriki kutoa fungu la kumi na kutoa sadaka maalum kupeleka neno la Mungu katika sehemu nyingine za nchi yetu na dunia.*

**Omba kwamba tutakuwa mawakili wema wa vitu vyote ambavyo Mungu ametupatia. Omba kwamba tutatumia karama zetu, uwezo, pesa na wakati wa kutumikia na kumheshimu. Omba kwamba tutakuwa mawakili wema wa karama ya Mungu ya upendo na wokovu. Omba kwamba tutashiriki karama zake na watu wengine. Omba kwamba tutatoa kwa hiari sadaka ambazo zitasaidia kueneza habari yake njema.**

- Soma Zaburi 78:1-8 na Shabaha ya Tano: *"Tutajaribu kuwafundisha watoto wetu na wengine juu ya Mwokozi wetu. Tutajitahidi kuongoza watoto na vijana kufahamu habari ya Kristo na jinsi ya kueneza Injili katika vyama vinavyokutana katika makanisa yetu."*

**Tuombe ili Mungu atusaidie "tukiwaambia kizazi kingine, Sifa za Bwana, na nguvu zake, na mambo yake ya ajabu aliyofanya." Tuombe ili tuweze kuwaongoza "Wamwekee Mungu tumaini lao" na "wazishike amri zake."**

**Kiongozi:** Tumalize mkutano wetu kwa kurudia kifungu chetu cha Ushirika wa Wanawake na kuimba wimbo wetu, *Nataka Nimjue*. Funga mkutano kwa maombi, mwombe Mungu aongoze Ushirika wako mnapojitahidi kuwa *"Wafanya kazi pamoja na Mungu."*

❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖ ❖

**Vifungu vya Kusoma Juma Hili:**
**Siku 1)** Wakolosai 3; **Siku 2)** 1 Wakorintho 13;
**Siku 3)** Wafilipi 2:1-18; **Siku 4)** Zaburi 1;**Siku 5)** Isaya 6:1-8;
**Siku 6)** Kutoka 3:1-14; **Siku 7)** 1 Samweli 3

UMOJA WA WANAWAKE MAKANISA YA WABATISTI

Wafanya Kazi pamoja na Mungu

1 Kor. 3:9

## Kadi za Kifungu cha Kukumbuka kwa kila soma

**Somo La Kwanza**

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."
Yohana 3:16

**Somo la Pili**

"Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu." Zaburi 119:105

**Somo la Tatu**

"Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani." Wakolosai 4:2

**Somo la Nne**

"Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu."
1 Wakorintho 4:2

**Somo la Tano**

"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?" 1 Wakorintho 3:16

**Somo la Sita**

"Na huu ndio upendo: tuenende kwa kuzifuata amri zake."
2 Yohana 6

**Somo la Saba**

"Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake."
1 Wakorintho 12:27

**Somo la Kumi na Tatu**

"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye." Wakolosai 3:17

**Somo la Kumi na Mbili**

"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."2 Timotheo 2:15

**Somo la Kumi na Moja**

"Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu."
1 Wakorintho 3:9

**Somo la Kumi**

"Mwe tayari sikuzote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu."
1 Petro 3:15

**Somo la Tisa**

"Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kama kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu."
2 Wakorintho 5:20

**Somo la Nane**

"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:19-20

# Mpango wa Mungu wa Wokovu

Vifungu vifuatavyo vya Biblia vinazungumzia **mpango wa Mungu wa wokovu** kwa wale ambao wamepotea. Vinaeleza ukweli ambao ni lazima mtu asikie na kukubali ili aokoke.

1) **Warumi 3:23** Ni lazima mtu huyo aelewe kwamba yeye ni mwenye dhambi na kwamba dhambi imemtenganisha na Mungu.

2) **Warumi 6:23** Ni lazima mtu huyo ajue kwamba mwenye dhambi amekabiliwa na mauti. Mungu hataki mtu ye yote atenganishwe naye. Anatoa zawadi ya uzima wa milele katika Yesu Kristo.

3) **Yohana 3:16** Mungu anatupenda na anatoa njia ya kutuwezesha kupata zawadi yake ya uzima wa milele. Ni lazima mtu amwamini Yesu ndipo apokee zawadi hii.

4) **1 Yohana 1:9** Ni lazima mtu akiri dhambi zake ndipo akubali mpango wa Mungu. Ni lazima atubu dhambi zake na amwombe Mungu msamaha. Ni lazima pia amwambie Mungu atawale maisha yake.

5) **Warumi 10:9-10** Ni lazima mtu huyo aamini kwamba Mungu amefanya kile alichoahidi. Ni lazima mtu huyo aamini kwamba amesamehewa dhambi zake na amepokea karama ya Mungu ya uzima wa milele.

Baada ya kutumia vifungu hivi, mwulize mtu huyo kama anaamini kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zake. Mwulize kama yuko tayari kufuata mpango wa Mungu wa wokovu. Ikiwa mtu huyo anataka kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi, mwambie aombe. Mwongoze anapompokea Yesu maishani mwake. Mwongoze anapomwomba Mungu msamaha wa dhambi zake na kumtaka atawale maisha yake.